VIZUIZI VYA MAFANIKIO

Sehemu ya Eneo Unaloishi

Soma Neno la Mungu
Na: Mwl, Mr. & Mrs. Steven Mwakatwila

UTANGULIZI

Watu wengi sana wanatafuta sana wafanikiwe sana, kila mtu mwenye akili timamu anataka kufanikiwa sana. Hata Mungu anataka ufanikiwe sana, Mungu anataka watoto wake tufanikiwe katika mambo yetu yote. Neno la Mungu linatufundisha wazi kuwa Mungu anataka tufanikiwe katika mambo yote tazama maneno haya ya Bwana yasemavyo,

"Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.
(3Yohana 1:1-2).

Maneno hayo ukiyaangalia utaona Mungu anataka tufanikiwe katika afya zetu, tufanikiwe katika uchumi wetu, tufanikiwe katika roho zetu,na katika mambo yako yote. Huo ndio mpango wake kwako na kwangu. Neno kufanikiwa maana yake ni kustawi au kuongezeka ama kukua, au kubarikiwa ama kupata heri. Watu wengi sana tunahitaji kubarikiwa sana kwa lugha nzuri niseme kupata mali. Naamini hata wewe ndugu yangu una nia hiyo ndani ya moyo wako. Moja ya maswali ambayo nimejiuliza miaka mingi sana, ni hili ikiwa Mungu anataka sisi watoto wake tufanikiwe ni kwanini hatufanikiwi kama Mungu atakavyo? Naamini hata wewe umekuwa na swali kama hili ndani ya moyo wako. Ndani ya somo hili Mungu atakufundisha mojawapo la tatizo ambalo linaweza kuwa ndio chanzo cha kutokufanikiwa kwako. Hebu tuanze kujifunza, naamini Roho Mtakatifu atakwenda kukufundisha vema kabisa.

VIZUIZI VYA MAFANIKIO YAKO

Mungu yupo tayari leo hii kuhakikisha watoto wake tunafanikiwa sana katika maeneo hayo yote, ndio maana leo hii ametupa somo hili,ili kila mtu atakaye kufanikiwa ahakikishe anayafanya hayo ambayo Bwana ameyaweka ndani ya moyo wangu na kunijalia neema ya kuyaandika na kuyasema kwa watoto wake ambao ni kanisa lake Mungu. Neno la Mungu linatufundisha wazi kuwa Mungu anataka watoto wake tupate faida kubwa. Ili tuzipate hizo faida anachofanya ni kutuletea mafundisho, Sikia maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Bwana mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli, asema hivi; Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata.
(Isaya 48:17a)

Ili tupate faida ni lazima tukubali kukaa darasani na kumruhusu Mungu Roho Mtakatifu atufundishe, na baada ya kutufundisha ni lazima tuhakikishe tunayashika yale aliyotufundisha, hapo ndipo tutakapo stawi sisi na watoto wetu. Tumekwenda sawa hapo?

Ukiwaangalia watoto wa Mungu wengi sana wanajua kuwa Mungu amewaahidi mafanikio, na wanaamini kabisa kuwa Mungu atawafanikisha sana au niseme atawabariki sana, lakini kila siku wanajikuta badala ya kufanikiwa ndio wanazidi kukwama na kuwa watu wenye uhitaji sana, neno uhitaji ni umaskini. Jambo hilo lilinisumbua sana, nilikuwa najiuliza maswali mimi mwenyewe binafsi kwa nini nimekwama kwenye eneo hili la kufanikiwa hasa kiuchumi, pia nilikuwa na waangalia ndugu zangu waliompokea Yesu kama Bwana na mwokozi wao walivyo, niliona kuwa wengi wanaishi maisha ya kimaskini sana, tofauti na kile ninacho kiona kwenye neno la Mungu, watoto wa Mungu wengi hawajafanikiwa katika uchumi wao, katika afya zao, wewe ona matatizo mengi ya kiafya yanavyo wakabili watoto wa Mungu, nimeona ndoa za watoto wa Mungu wengi hazina mafanikio kama Mungu alivyo sema tufanikiwe katika mambo yote. Nimeangalia na kuwaona watoto wa waliookoka wanavyosoma au wanaposomea nikaona kuwa wengi wanasoma katika shule zisizo na sifa, kutokana na gharama kubwa zilizopo kwenye shule zenye sifa watoto wa Mungu wengi kutokana na tatizo la uchumi hawawezi kuwapeleka watoto wao kwenye shule hizo zenye sifa, wewe angalia uone hili ninalo kuambia utaona wazi kuwa watoto wa waliookoka wengi sana wapo nyumbani baada ya kumaliza elimu ya msingi. Wanataka sana kufanikiwa kielimu lakini wazazi hawana uwezo wa kuwasomesha, wanajikuta wapo nyumbani. Tazama leo jinsi elimu ya juu ilivyo ghali umewahi kuliangalia hili na kujiuliza je! Kama hali ya kiuchumi ndiyo taabu kwa watoto wa Mungu unafikiri tutakuwa na watoto wetu wangapi watakao kuwa na elimu ya juu? Na hao ndiyo wanapaswa kuwa viongozi wa nchi hii.

Wewe ona hata nyumba tunazo ishi, utaona asilimia kubwa ni nyumba za kupanga, hata kodi zenyewe ni shida kulipa katika majira yake, ona mavazi tuya vaayo sisi na watoto wetu yalivyo. Ona chakula tunacho kula nk, tazama mafanikio ya kihuduma au tumezoea kuita kiutumishi yalivyo, utaona watumishi wengi huduma zao kwa kweli zimekwama. Wanajitahidi sana lakini wapi ukiyaangalia haya kwa kutulia utaona watoto wa Mungu wengi hawajafanikiwa kama Mungu atakavyo tufanikiwe. Nikawa na maswali mengi sana, ni kwa nini? Tatizo liko wapi? Namshukuru Mungu aliyenipatia mafundisho haya, aliponifundisha mimi, na mimi nikaanza kuyafanyia kazi, kweli nikaona mabadiliko katika maisha yangu, ya kiroho, kiutumishi, hata kiafya na kiuchumi.

Sasa leo hii tutaanza kuangalia kwa upana vizuizi vikubwa ambavyo leo hii vinaweza kuzuia mafanilio yako ya kiuchumi – Kiroho –kiutumishi na kiafya. Hebu tuone kizuizi cha kwanza nacho ni:

ENEO UNALO ISHI

Kila mtu anaemwamini Yesu Kristo kama ni Bwana na Mwokozi lazima ufahamu kuwa mafanikio yako ya Kiuchumi, Kiafya na hata Kiroho hata kiutumishi na mambo yako

mengine yote, yanatokana na eneo unalo ishi. Fahamu ukikosea suala la eneo la kuishi, unaweza kabisa kupoteza baraka zako zote ambazo Mungu alikupangia uwe nazo. Kwa bahati mbaya Wakristo wengi hawalijui jambo hili, na kwa kuwa hawalijui, hawaliombei kwa Mungu, pia hawajui namna ya kufanya ili kulifanya eneo hilo wanaloishi liachilie kila baraka ambazo Mungu ameziweka hapo kwa ajili ya watoto wake waliopewa kibali na Mungu cha kuishi hapo.

MUNGU NA IBRAHIMU

Ukisoma maandiko matakatifu utaona wazi kuwa mafanikio ya watu wa Mungu wote yanapatikana baada ya wao kuishi mahali ambapo Mungu aliwapangia kuishi kwa muda aliotaka waishi hapo. Ukisoma maandiko matakatifu utagundua wazi kabisa kuwa,Mungu alipoamua kumfanikisha Ibrahimu alianza kwanza kulishughulikia eneo ambalo Ibrahimu alipaswa aishi. Na alipokutana kwa mara ya kwanza na Ibrahimu alianza kumfundisha mambo mengi sana, moja ya jambo ambalo Mungu alimfundisha Ibrahimu lilihusu eneo ambalo Ibrahimu anapaswa kuishi, Biblia inatufundisha katika kitabu cha (Mwanzo 12:1-3) sikiliza maneno haya ya Bwana yanasema hivi. “Bwana akamwambia Abramu, toka katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba yako, uende mpaka nchi nitakayo kuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.”

Ukiyaangalia maneno hayo hapo utaona kuwa, Mungu alipanga mpango wa kumfanikisha Ibarahimu, Kizuizi cha kwanza ambacho Mungu aligundua kuwa kinaweza kuzuia mafanikio ya Ibrahimu kilikuwa ni eneo analo ishi. Mungu akaanza kumfundisha Ibrahimu na kumwambia inampasa atoke katika eneo hilo analo ishi. Eneo ambalo yeye Ibrahimu alilizoea sana, fahamu alizaliwa hapo na hapo ndipo alipokulia na kuoa hapo, pia eneo hilo lilikuwa na jamaa zake au ukoo wake. Fahamu mahali hapo ndipo Ibrahimu alipokuwa na urithi wake kutoka kwa baba yake. Sehemu hiyo ndiyo ambayo alijenga nyumba yake na kuishi huko miaka mingi sana pamoja na mke wake Sara. Lakini Mungu aligundua kuwa eneo hilo ndilo kikwazo cha mafanikio ya Ibrahimu. Akaamua kumtoa hapo na kumpeleka sehemu ambayo Mungu alijua kuwa kama Ibrahimu atakaa hapo ndipo atakapo fanikiwa sana katika mambo yake yote, pamoja na uzao wake. Sikia alimwambia akienda huko hapo ndipo atakapokuwa baraka, jiulize swali hili Hivi Ibrahimu asingekuwepo katika eneo hilo alilofundishwa na Mungu aende, je! Angekuwa baraka? Jibu ni rahisi asingekuwa baraka wala asingezipata hizo baraka alizoahidiwa na Mungu.

TATIZO KUBWA LEO HII

Watoto wengi sana wa Mungu leo hii wamejikuta wamekwama na wanatafuta njia ya kujikwamua katika eneo la kukwama kwao kimafanikio katika mambo yao yote

lakini kila wanapo jitahidi wanajikuta wamekwama. Wanakesha kwenye maombi, wanaombewa na watumishi mbalimbali,wanatoa zaka nk, lakini wanajikuta wakizidi kukwama katika mambo yao yote. Sikiliza moja ya kizuizi kilichozuia baraka zao ni hiki cha eneo wanaloishi. Watoto wa Mungu wengi sana hawajui kuwa mafanikio yao yatakuja kwa sababu ya eneo wanalo ishi na mabaya yatakuja kwa sababu ya eneo wanalo ishi. Fahamu ndugu kama utakosea eneo la kuishi utapata shida sana hata kama umeokoka, bahati mbaya sana suala hili watoto wa Mungu wengi hawalijui, hawaombi, hawatafuti kwa kupitia maombi kujua ni wapi Mungu kawapangia waishi. Watoto wa Mungu wengi sana wamejikuta hawana mafanikio kiroho, au kiuchumi, kiafya na kiutumishi, unajua ni kwa sababu gani? ni kwa sababu wanaishi mahali ambapo pamewakaba, nataka ujue kuwa mafanikio yako yanatokana na eneo unalo ishi.

Sasa kama mafanikio yako yatatokana na eneo unalo ishi basi unatakiwa uwe mwangalifu katika jambo hili kuliko ulivyokuwa zamani, watu wengi hatujui kuwa jambo hili Mungu ndiye anahusika nalo sana, fikiri Mungu ndiye aliyehusika na eneo ambalo Ibrahimu anatakiwa aishi, kumbuka Mungu ni yeye yule jana leo na hata milele, kama siku ile alihusika na suala la eneo la kuishi Ibrahimu ili awe na mafanikio fahamu hata leo anataka ahusike na eneo unalotakiwa uishi wewe, iwe kwa muda au utakaloishi mpaka siku ya kufa kwako ili uwe baraka.

MFANO KUISHI KIMAZOEA

Wewe ona watu wengi leo wanaishi maeneo fulani kwa sababu ya mazoea, yaani anaishi hapo kwa sababu eti hapo ndipo alipozaliwa, au ndiyo nyumbani kwao au hapo ndipo anapopaona yeye kuwa kuna biashara nzuri nk. Kwa sababu hizo ana amua kuishi hapo, sikiliza Mungu hakuangalia Ibrahimu hapo ndipo alipozaliwa au ndipo kwenye jamaa zake aliamua kumwondoa hapo ili apate mafanikio. Sikiliza ukikosea eneo la kuishi hutapata mafanikio, watu wengi sana leo hii wamejenga nyumba au kuhamia katika nyumba za kupanga pasipo kumshirikisha Mungu. Matokeo yake waliko jenga au kupanga wamejikuta hawana mafanikio kama si katika uchumi basi Kiroho na kama sio kiroho basi kiafya na hata kiutumishi. Lazima uwe makini mpendwa katika suala hili. Ngoja nikuulize unapoenda kujenga hapo upaonapo wewe kuwa panafaa, unajua Mungu amepanenea nini mahali hapo? au amebatiliza uovu wa namna gani mahali hapo?. Ukisoma maandiko matakatifu utaona kuna maeneo ambayo Mungu ameyalaani, kwa sababu za maovu ambayo watu wa maeneo hayo au walioishi hapo kwanza waliyafanya.

LAANA YA ARDHI

Sikiliza, neno la Mungu linatufundisha kuwa, Mungu anatabia ya kuachilia laana katika ardhi kutokana dhambi za watu wa mahali hapo walizo zifanya, kwa hiyo unapoenda kujenga pasipo maongozi ya Mungu unaweza kukutana na madhara au laana ambayo ardhi hiyo imebeba. Hebu angalia mifano hii, sikia maneno haya

"Naye Yoshua akawaapisha kiapo wakati ule, akisema, na alaaniwe mbele za Bwana mtu yule atakayeinuka na kuujenga tena mji huu wa Yeriko; ataweka msingi wake kwa kufiwa na mzaliwa wa kwanza wake, tena atayasimamisha malango yake kwa kufiliwa na mtoto wake mwanamume aliye mdogo, basi Bwana alikuwa pamoja na Yoshua; sifa zake zikaenea katika nchi ile yote."
(Yoshua 6:26-27).

Umeyasikia maneno hayo mpendwa? Eneo hilo lote lililaaniwa,fikiria wewe umeenda kujenga kwenye eneo hilo ingawa umeokoka unafikiri utapona? Ndio maana nakuambia ukweli kuwa suala la wewe kuishi eneo fulani si la kujikurupukia tu, lazima ujifunze kufanya maombi ili Mungu ashughulikie eneo unalotakiwa uishi, iwe kwa muda au kwa siku zote ulizopewa na Bwana kuishi hapa duniani. Neno la Bwana linasema eneo hilo lililaaniwa, nakuambia ukweli hata leo hii kuna maeneo ambayo yamebeba laana fulani, usipokuwa mwangalifu ukaenda kujenga huko au kupanga huko utakutana na shida nyingi zisizoisha, mpaka utapopata ufahamu kuwa kinachopelekea upate shida hizo ni hilo eneo.

Wewe hujaona leo hii mtu alikuwa mzima kabisa, akihamia kwenye nyumba yake aliyoijenga au akahama mtaa fulani akaenda mtaa fulani, anaumwa au anakufa, kama si yeye mke au watoto wake. Watu hawamuulizi Mungu ni kwanini kumetokea hivyo, wengi hukimbilia kusema ni majaribu mpendwa. Wewe ona kuna watu wanakuwa na afya nzuri sana rohoni, lakini wakihamia eneo fulani tu, afya yao ya kiroho huwa mbaya sana, wanajiuliza ni kwanini lakini hawajui ni kwa nini, sikiliza ukikosea eneo haya yanaweza kukukuta.

Ngoja nikuulize swali unajua ni kwa nini unaumwa-umwa? nani amekuambia uishi kwenye nyumba hiyo unayoishi? Unaijua hiyo nyumba? wewe unalala tu, hujui ardhi hiyo unayoilala imenenewa nini na Mungu au na huyo mwenye nyumba. Mfano leo hii inawezekana unashinda hospital unaumwa mara kwa mara, inawezekana tatizo hilo chanzo chake ni hiki ninachokuambia umekosea eneo unaloishi. Nina mfano hai wa ndugu yangu mmoja ambaye alikuwa kila mara analazwa hospitali Tukuyu, yaani ilikua haiwezi ikapita miezi sita hajalazwa hospitali, ilifikia hata watoto wake wakaizoea hali ile, na kuona ni jambo la kawaida tu, nakumbuka mama huyo alifahamiana na wauguzi na wagaga wa hiyo hospitali utafikiri hata yeye ni mfanyakazi wa hiyo hospitali.

Hata watoto wake pia walikuwa wakifahamiana sana na wauguzi wa hospitali ile. Siku mume wake alipopewa uamisho wa kwenda Mtwara mama yule ndiyo ikawa pona yake. Alipohamia huko tu, magonjwa yakamwachia kabisa. Leo hii ukimuona huwezi amini kama ndiye mama yule aliyekuwa kila mara akisumbuliwa na maradhi hasa ya tumbo. Leo kapona ni mzima wa afya njema kabisa, siku Mungu ananifundisha somo

hili nilishangaa akanikumbusha habari za miaka iliyopita za huyo mama, nikagundua kuwa kilichopelekea mama yule kuugua mara kwa mara kilikuwa ni eneo alilokuwa akiishi huko Tukuyu, fikiri mama huyo Tukuyu ndio nyumbani kwao, lakini alikuwa anaumwa kila mara, mara tumbo, mara kichwa mara anatapika sana, yaani ilikuwa vurugu tupu. Hata leo hii akienda Tukuyu kusalimia ndugu zake, akikaa siku chache tu, lazima aumwe, mafanikio ya afya yake yalipatikana pale alipoondoka katika eneo lile. Naamini umeuelewa mfano huo.

Ngoja nikupe mfano wa pili, Lutu alipokosea kuchagua eneo la kuishi alipata shida sana, Lutu alijichagulia eneo la kuishi, hakumshirikisha Mungu katika jambo hilo, alijifanyia mwenyewe matokeo yake yakamkuta mambo makubwa sana, hakufanikiwa katika maisha yake yote sikiliza maneno haya ya Mungu yanavyotufundisha

"Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya Bwana, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari, Basi Lutu akajichagulia Bonde la Yordani; ……. Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi; maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele." (MWANZO13:11-15).

Neno la Mungu linasema Lutu alijichagulia yeye mwenyewe eneo la kuishi, Ibrahimu alichaguliwa eneo la kuishi na Mungu, umeona tofauti yao? Lutu alichaguliwa eneo la kuishi pasipo mwongozo wa Mungu aliliona eneo lile kwa macho ya kibinadamu akaamua kuishi huko, Ibrahimu alichaguliwa eneo lile na Mungu. Fuatilia sasa maisha ya Lutu baada ya kukosea eneo la kuishi jinsi yalivyo kuwa ya taabu, Biblia inasema alipoenda huko alipata shida sana kiroho kiuchumi hata kiafya, Lutu alipokosea alipata shida kiroho, neno la Bwana linasema miaka yote aliyoishi Sodoma na Gomora alipata shida kiroho angalia maneno haya ya Bwana yanavyosema juu ya jambo hili nikuambialo.

"... Akamwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu". (1PETRO 2: 7).

Afya ya Lutu ya kiroho haikuwa nzuri tokea alipokwenda Sodoma na Gomora, neno linasema maisha yake ya kiroho yalijaa huzuni, ninacho amini ni kuwa furaha ya rohoni inaleta afya ya moyoni mpaka kwenye mwili yaani ndani ya mifupa, sikiliza neno la Bwana lisemavyo

"Moyo uliyochangamka ni dawa nzuri; bali roho iliyopondeka huikausha mifupa" (MITHALI 17:22).

Lutu hakuwa na afya nzuri rohoni mwake, kwa kuwa hakuwa na furaha moyoni mwake, kama alikosa furaha moyoni basi roho yake ilipondeka, yaani mafanikio ya afya ya roho ya Lutu ilikuwa mbaya, neno linaiita ilipondeka. Fahamu roho ikipondeka mifupa inakauka, mwenyewe ona jinsi huyo Lutu alivyokuwa na afya mbaya ya mwili wake, kisa alikosea kuchagua eneo la kuishi yeye na familia yake na mali zake. Lutu alihuzunika miaka yote, aliyokaa kule, mafanikio yake ya kiroho hayakuwa mazuri, naamini alinajisika sana kutokana na eneo hilo alilokuwa akiishi hakuwa na amani katika maisha yake yote wala hakuwa na furaha ya kufurahia maisha. Narudia tena, kisa alikosea eneo la kuishi inawezekana hata wewe huna kabisa furaha moyoni mwako ingawa umeokoka, lakini ni mtu mwenye huzuni tena umejaa hofu na mashaka unajua ni kwa nini? Inawezekana unaishi eneo ambalo Mungu hakutaka uishi, inawezekana hata maendeleo yako ya kiroho yanafishwa na hilo eneo unaloishi.

Lutu alipokosea kuchagua eneo la kuishi alijikuta akipata misukosuko ya kiuchumi, alipoteza mali zake zote. Mara ya kwanza alipoteza mali zake pale alipovamiwa na maadui waliokwenda kupigana na watu wa Sodoma na Gomora, hata yeye akatekwa**,** sikiliza maneno haya yanatupa habari hii kwa uzuri kabisa

"……wakachukua mali zote za Sodoma na Gomora na vyakula vyao vyote, wakenda zao. Wakamtwaa Lutu mwana wa nduguye Abramu, aliyekaa huko Sodoma, mali yake, wakaenda zao."
(Mwa 14:8-11)

Bahati yake Ibrahimu alikwenda kumuokoa, neno linasema Ibrahimu alienda kumuokoa.

"Mtu mmoja aliyeponyoka akaenda akampasha habari Abramu Mwebrania; naye amekaa panapo mialoni ya mamre, yule Mwamori ndugu ya Eshkoli, na ndugu ya Aneri, na hao walikuwa wamepatana na Abramu. Abramu aliposikia ya kwamba nduguye ametekwa mateka akawapa silaha vijana wake, waliozaliwa katika nyumba yake, watu mia tatu na kumi na wanane, akawafuata mpaka Dani. Akajipanga apigane nao usiku, yeye na watumwa wake, akawapiga, akawafukuza mpaka Hoba ulioko upande wa kushoto wa Dameski. Naye akarudisha mali zote, akamrudisha na Lutu nduguye na mali zake, na wanawake pia, na watu."
(MWANZO 14:13-16).

Lutu akajikuta akipoteza tena mali zake zote, safari hii ya pili ni pale Mungu alipoamua kuichoma moto Sodoma na Gomora, kumbuka Lutu alipokuwa anatolewa Sodoma alitolewa yeye na watoto wake tu, hakufanikiwa kukimbia na mali zake, alipoteza zote, umewahi kujiuliza ni kwanini umepoteza mali zako zote angalia mahali unapoishi? Sikiliza, Lutu alipoteza kila kitu kuanzia nyumba, mashamba, nk, Leo hii watu wengi hujikuta wakipoteza mali zao nyingi, na wakipoteza hawajui kisa ni nini, wengi hukimbilia kumpinga shetani, kumbe si shetani ila ni Mungu kaamua kuupiga huo mji

au hilo soko, na matokeo yake watoto wa Mungu walioweka biashara zao katika mji huo wanajikuta wakipata hasara nyingi sana, wewe ona leo watoto wa Mungu wengi, wameweka maduka katika maeneo fulani bila kibali kutoka kwa Mungu, maana yangu hawakumuomba Mungu awape muongozo wa kuyajenga hayo maduka. Ila waliona maeneo hayo kuwa ni mazuri kibiashara, kumbe kesho maeneo hayo Mungu ataruhusu yateketezwe kwa moto ambao hata watu wazima moto hawawezi kuuzima. Ndipo watoto wa Mungu waliowekeza mali zao hapo wanapojikuta wakiingia umasikini mkubwa, sikiliza ukikosea eneo la kuishi yanaweza kukukuta mambo kama hayo yaliyomkuta Lutu.

Lutu alipokosea kuchagua eneo la kuishi, alijikuta akimpoteza hata mke wake

" Lakini mkewe mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi" (Mwanzo 19:23-38).

watu wengi husema " mke wa Lutu alikosea sana". sikiliza ni kweli yule mama alikosea kwa kugeuka nyuma, au kwa lugha nzuri aligeuka autazame mji, kwanini yule mama alitazama nyuma? Naamini alikuwa na mapenzi makubwa na huo mji, kuna mambo ambayo yalimjaa moyoni aliyoyapokea kutokana na tabia ya huo mji, swali langu ni hili, ni nani alimpeleka huyo mwanamke kwenye huo mji? Jibu ni Lutu, Lutu ndiye anayepaswa kubeba lawama zote za kupotea kwa mke wake, fikiri, kama Lutu angelimuomba Mungu mapema ampe eneo ambalo Mungu anataka Lutu na familia yake waishi naamini Mungu angempa eneo hilo, na hayo mabaya yasinge mkuta.

Leo hii watu wengi wamewapoteza waume zao kisa ni pale walipokosea katika eneo la kuishi, wakaishi sehemu ambayo Mungu hakuwaambia waishi hapo, matokeo yake wakajikuta waume zao wamepotelea kwa Malaya au ulevi nk, fahamu ukikaa katika mji fulani utakutana na tabia za huo mji na marafiki, nk, sasa kama mume wako hana upako wa kukaa hapo, nakuambia ukweli hatapona katika eneo la uzinzi hata kama ameokoka! Watu wengi wamejikuta walipojenga nyumba au kupanga maeneo fulani ndipo wake zao walipobadilika tabia, wanawake hao wakajikuta wanakuwa na tabia mbaya, iliyopelekea hata ndoa yao kuvunjika, jiulize swali mbona mlipokuwa kule kabla hamjaja hapo mkeo hakuwa na tabia hiyo aliyo nayo sasa? nini kimembadilisha? Sikia eneo linaweza kumbadilisha mkeo.

Ukikosea eneo la kuishi nakuambia ukweli unaweza kumpoteza mkeo kabisa, ona mfano huu, Ibrahimu aliponea chupuchupu kumpoteza mkewe Sara kisa ni kutokana na eneo alilokwenda, anadai lilikuwa halina hofu ya Mungu. Wewe isome habari hii yote katika kitabu cha (MWANZO 20 :1-18), Mimi nikupe mstari huu ambao nimeuona unaweza kukusaidia sana kujua kuhusu ukikosea eneo la kuishi unaweza kumpoteza mkeo, ona maneno haya ya Ibrahimu yasemavyo.

"Abimeleki akamwambia Ibrahimu, umeona nini hata ukatenda jambo hili? Ibrahimu akasema, kwa sababu naliona yakini hapana hofu ya Mungu mahali hapa, nao wataniua kwa ajili ya mke wangu"
(Mwanzo 20:10-11)

Ibrahimu alililona eneo hilo kuwa halina hofu ya Mungu, kwanini aliamua kukaa hapo? Fikiri aliliona kabisa eneo hilo kuwa si zuri kwake na kwa mke wake, kwanini aliamua kukaa hapo? Leo ndivyo ilivyo kwa watu wengi wanajua kabisa kuwa maeneo wanayoyaendea kukaa iwe kwa kupanga au kujenga hayana hofu ya Mungu yanaweza kupelekea hata ndoa zao kuvunjika lakini wako kama Ibrahimu, wako tayari kukubali wake zao wapotee kwa sababu ya faida fulani waionayo katika mji huo au eneo hilo, Mungu alimsaidia Ibrahimu, sijui kwako mpendwa, kila mtu ana bahati yake, nakushauri uwe mwangalifu katika suala hili, anza kuomba leo kuhusu eneo ambalo Mungu anataka uishi.

Lutu baada ya kutolewa Sodoma na Gomora, alifanya kosa kama hilo tena, alikosea eneo ambalo Mungu alitaka akae, na alipokosea alijikuta anawakosesha hata watoto wake wakike, wakazini na baba yao, unajua kilichopelekea wazini na baba yao kilikuwa ni nini? Sikiliza kilikuwa ni eneo wanaloishi! Ona maneno haya ambayo Mungu alimwambia Lutu ayafanye lakini Lutu akajitetea.

"Ikawa walipomtoa nje, mmoja alisema, jiponye nafsi yako; usitazame nyuma, wala usisimame katika hilo bonde popote; ujiponye mlimani, usije ukapotea. Lutu akamwambia, sivyo bwana wangu! Tazama, mtumwa wako ameona kibali machoni pako, nawe umezidisha rehema zako ulizonifanyia kwa kuniponya nafsi yangu, nami siwezi kukimbilia mlimani nisipatwe na yale mabaya, nikafa. Basi mji huu u karibu niukimbilie, nao ni mdogo, nijiponye sasa huko, sio mdogo huu? Na nafsi yangu itaishi. Akamwambia, tazama, nimekubali hata kwa neno hili, kwamba sitauangamiza mji huo uliounena. Hima ujiponye huko, maana siwezi kufanya neno lolote, hata uingiapo humo. Kwa hiyo jina la mji ule likaitwa Soari"
(Mwanzo 19:17-22)

Umeyaona maneno hayo jinsi yanavyo sema? Lutu alifanya kosa kama lile la kwanza, alijichagulia eneo la kukaa yeye kwa mapenzi yake. Aliambiwa aende mlimani akakae huko, yeye akajitetea kuwa hawezi kukimbilia huko, ngoja nikuulize swali, hivi ! Mungu alikuwa hajui kuwa Lutu hawezi kukimbilia mlimani? Mimi na amini Mungu alijua kuwa Lutu alikuwa na uwezo wa kwenda mlimani, ila yeye Lutu aliamua kujitetea, Mungu akamruhusu aende kwenye mji huo aliouona yeye kuwa unamfaa. Sikia kivumbi chake kilicho mkuta huko aliko kimbilia, neno la Mungu linasema aliishia kufanya tendo la ndoa na watoto wake kisa, eneo hilo lilikuwa halina wanaume, ona maneno haya yanavyo tufundisha

"Lutu akapanda Soari akakaa mlimani, na binti zake wawili pamoja naye, kwa sababu aliogopa kukaa katika Soari. Akakaa katika pango yeye na binti zake wawili. Yule mkubwa akamwambia mdogo wake. Baba yetu ni mzee, wala hakuna mtu mume katika nchi atuingie kama ilivyo desturi ya dunia yote. Haya, na tumnyweshe baba yetu mvinyo tukalale naye, ili tumhifadhie baba yetu uzao. Wakamnywesha baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka huyo mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo, Tazama, nimelala jana na baba yangu, tumyweshe mvinyo tena usiku huu, ukaingie ukalala naye. Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala kuondoka. Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao."
(Mwanzo 19:30-36)

Umeyaona maneno hayo? Kilichopelekea hao watoto kufanya hayo waliyoyafanya kilikuwa ni kwa sababu ya eneo hilo walilopelekwa na baba yao huyo lilikuwa halina wanaume. Siufurahii ubaya wa hao watoto walioufanya, ila najaribu kukuonyesha picha hiyo uone umuhimu wa kumuomba Mungu sana kuhusu eneo utakalo ishi wewe na mkeo na watoto wako, kama ukikosea unaweza kutofanikiwa kiroho, kiuchumi, kihuduma, hata kiafya, pia unaweza kuwasababishia watoto wako wajifunze kufanya mambo mabaya, watoto wanaweza kupotea kitabia kwa sababu tu, baba umewapeleka sehemu mbaya ya kuishi. Sikiliza sasa nikuambie ukikosea eneo la kuishi yatakutokea kama ya Lutu unaweza kupoteza mali zote pili unaweza kupoteza ndoa yako unaweza kupoteza watoto wako kwa sababu umekosea eneo la kuishi. Ngoja ni kuulize swali hili, unaishi wapi au unataka kuishi wapi? Nani amekuambia uishi hapo? Nakushauri usiishi sehemu kwa sababu zako wewe binafsi, tafuta muongozo kutoka kwa Mungu umenielewa? Tusonge mbele.

MFANO WA WANA WA ISRAEL KWENDA MISRI

Katika sehemu iliyotangulia tumeanza kuona kuwa Mungu anataka ufanikiwe sana katika mambo yako yote, na tumeanza kuona moja ya kizuizi kinacho weza kuzuia mafanikio yako ni pale unapokuwa umekosea eneo lako kuishi. Tumeona wazi kuwa Mungu anahusika sana na maisha ya kila mtu, kila mtoto wa Mungu lazima atambue kuwa inampasa kujua kuwa katika suala la kuishi kwake hapa duniani anahijitaji mwongozo kutoka kwa Mungu. Kwanini nakuambia hivyo sikia, Mungu ndiye aliyekuleta hapa duniani, na alipokuleta hapa duniani, kuna mipango mingi aliyo kupangia, anayo tayari, sikiliza maneno haya ya Mungu yasemavyo

"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho"
(YEREMIA 29:11)

Nilipo yasoma maneno hayo kwa lugha ya kiingereza nikapata maana nyingine nzuri zaidi, yanasema hivi.

"For I know the plans I have for you, declares the LORD, Plans to prosper you and not to harm you, plans to give you hope and a future"
(JEREMIAH 29:11).

Kumbe Mungu anayo mipango aliyoipanga kwa ajili yako. Kama ana mipango aliyoipanga kwa ajili yako fahamu hata sehemu unayopaswa kuishi aliisha ipanga tayari. Yeye ndiye anayeijua sehemu ya kuishi wewe iko wapi. Ndiyo maana nakuambia unatakiwa uhakikishe unakuwa na tabia ya kumuomba Mungu kuhusu eneo alilokupangia uishi. Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Mungu anasema kuwa anayo mipango ya mafanikio yako, kumbuka mafanikio yako yanategemea pia eneo unaloishi. Eneo linaweza kupitisha mafanikio ya mtu.

Sikiliza Mungu alihusika sana na anahusika sana na tendo hili la watoto wake waishi wapi na kwa muda gani.Ona mfano huu mzuri, Mungu alimwambia Ibrahimu kuhusu habari za uzao wa Ibrahimu waishi wapi, na kwa kipindi gani

"Bwana akamwambia Abramu, ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne. Hata na taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi. Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani, utazikwa katika uzee mwema. Na kizazi cha nne kitarudi hapa, maana haujatimia uovu wa Waamori bado."
(Mwanzo 15:8-21)

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi kuwa Mungu alimwambia Ibrahimu mapema habari za uzao wake watakaa wapi na kwa muda gani. Na hivyo ndivyo Mungu alitaka hao watoto wa Ibrahimu wakae huko Misri miaka mia nne, yaani ni kwa muda, tena ni muda ambao Mungu mwenyewe aliupanga wakae huko. Na baada ya miaka hiyo mia nne atawarudisha kwenye eneo alilowapangia yeye waishi hapo mpaka mwisho wa dunia.Hebu fikiri, Mungu aliongea na Ibrahimu habari za miaka mia nne ya kukaa kwa uzao wa Ibrahimu Misri. Hapo unaona namna Mungu anavyo husika katika habari za watoto wake waishi wapi na kwa muda gani.

Hata leo hii Mungu ametupa maneno hayo anataka kutufundisha hata sisi kuwa tunatakiwa kujua mpango wa Mungu wa kukaa kwetu kwenye maeneo maalum aliyotupangia tuyakae. Mungu aliamua kuwafundisha wana wa Israeli kuwa kila Mwisraeli aishiye Misri na kujenga huko lazima ajue wazi kuwa hapo wanakaa kwa muda tu. Iko siku watahama, Mungu aliamua kuwapa taarifa mapema kuwa hata nyumba watakazo jenga wajue wanazijenga ni za muda tu, kila kitu watakacho kifanya hapo ni cha muda tu si cha kudumu. Leo hii watoto wa Mungu wengi wamepoteza

mafanikio yao kwa kutofahamu kuwa wanatakiwa waishi hapo wanapoishi kwa muda gani.

Wewe hujawahi ona mtu anaishi mji fulani anapata fedha anaamua kujenga hapo nyumba ya kuishi, hana mawasiliano na Mungu wake, ila maombi ayaombayo anamuomba Mungu amjengee hapo, wakati Mungu hajamwambia au hajapanga huyo ndugu ajenge hapo,Yeye anaanza kuijenga hiyo nyumba.Sikiliza,kabla hajaimaliza anapewa uhamisho, kinachotokea anaiuza hiyo nyumba isiyoisha kwa bei ya hasara sana. Wana wa Israeli walikwenda Misri wakiwa na ufahamu kuwa huko hawatakiwi kuishi maisha yao yote, na aliye wapeleka huko alikuwa ni Mungu, swali langu kwako ni hili, unaishi wapi? Nani kakuambia uishi hapo? Unajua muda wa kukaa hapo? Inawezekana wewe ni mfanyakazi umehamishiwa hapo, sikia usikurupuke kujenga hapo nyumba ya kuishi kama huna kibali kutoka kwa Mungu, anza kuomba leo Mungu akuwezeshe kuishi mahali pale anapotaka uishi.

Ona mfano huu mwingine Wana wa Israeli walimkorofisha Mungu, Mungu akawapa adhabu ya kutawaliwa na Mfalme wa Babeli, akawatoa wana wa Israeli katika nchi yao, akawapeleka huko Babeli, neno la Mungu linasema Mungu alipanga wakae huko kwa muda wa miaka sabini

"Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danieli, kwa kusoma vitabu nilifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la Bwana lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini."
(DAN 9:)

Miaka sabini ni umri wa mtu mzima, sasa hebu fikiria kama hawa wana wa Israel wasingefahamu kama wanatakiwa wakae hiyo miaka sabini huko Babeli, na baada ya miaka hiyo sabini ndio Mungu awarudishe kwenye nchi yao ya ahadi, si mpaka leo hii wangekaa huko huko Babeli? Naamini wasingelijua hilo wangekuwa Babeli mpaka leo. Sikiliza ni nachotafuta nikujengee katika ufahamu wako ujue na ufahamu kuwa Mungu anahusika sana na jambo hili la wewe kuishi wapi ukikosea tu utapata taabu sana wewe na uzao wako.

Ukiyasoma maandiko matakatifu utaona wazi kuwa mafanikio ya watu wengi ndani ya Biblia yalitokea baada ya wao kuongozwa na Mungu wakae wapi. Ona mifano hii.

MFALME DAUDI

Kila mtu asomae maandiko matakatifu anajua kuwa Mfalme Daudi alifanikiwa katika mambo yake mengi.Unajua moja ya siri ya mafanikio ya Mfalme Daudi ilikuwa ni kutafuta muongozo kwa Bwana Mungu ni wapi anapaswa akae na kwa kipindi gani. Mfalme Daudi hakujichagulia mahali pa kuishi ovyo ovyo, aliomba na kupata muongozo

kutoka kwa Mungu ona maneno haya yasemavyo

"Ikawa baada ya hayo, Daudi akauliza kwa Bwana, akasema, je! Niupandiye mji wowote wa Yuda? Bwana akamwambia, haya! Panda. Daudi akasema, niupandie mji upi? Akasema Hebroni. Basi Daudi akapanda aende huko, pamoja na wakeze wawili, Ahio wa Yezreeli, na Abigaili, mkewe Nabali, wa Karmeli. Daudi naye akawapandisha watu wake walikuwa pamoja naye, kila mtu wa nyumba mwake; nao wakakaa katika miji ya Hebroni. Basi watu wa Yuda wakaenda, wakamtia Daudi mafuta huko, awe Mfalme juu ya nyumba ya Yuda.
(2Samweli 2: 1-4).

Mfalme Daudi alimuuliza Mungu ni wapi anatakiwa aishi, Mungu akamwambia Hebroni, alipoenda Hebroni mafanikio yakamfuata huko huko, neno linasema akafuatwa na watu wa Yuda na wakampaka mafuta ya kuwa Mfalme. Fikiri kwanini hapo kwanza hao watu hawakumfuata na kumtia mafuta?unajua Daudi alipoambiwa na Mungu aende Hebroni huko ndiko mafanikio yake yalipoanza kuchanua. Swali langu kwako ni hili, Wewe unakaa wapi? nani alikwambia ukae hapo? Ngoja nikupe mfano huu, baba yangu alijenga nyumba yake Tukuyu, na alipanga kuishi huko pale atakapostaafu kazi, mimi niliifahamu hiyo mipango ya baba yangu. Siku moja, Mungu alisema na mimi na kunituma niende nimwambie baba yangu kuwa, ameamua yeye kumjengea baba yangu nyumba Mbeya mjini kwa utukufu wake Mungu. Mungu aliniambia nimwambie baba yangu aishi Mbeya wala si Tukuyu, unajua baba yangu alikuwa amejenga Tukuyu eneo la Katumba, huko ndiyo nyumbani kwetu kiuokoo. Lakini mpango wa Mungu ulikuwa tofauti kabisa na mpango wa baba yangu, baba alikuwa na mji mkubwa huko Katumba. Nilifunga safari mpaka Mbeya alikokua baba yangu anafanyia kazi, nikampa baba ujumbe huo toka kwa Mungu, nashukuru sana, baba alikubali, kweli baba hakuwa na uwezo wa kujenga nyumba nyingine mjini Mbeya kwa kipindi hicho nilipo mpelekea ujumbe huo, Sikia, Mungu kwa muujiza wake alimjengea baba yangu nyumba nzuri tena kubwa sana. Na baada ya kuishi hapo akamjengea nyumba nyingine nzuri sana ya kisasa eneo la Forest mpya.

Sisi katika familia ya baba yetu tunamshangaa sana Mungu kwa hayo aliyomfanyia baba yetu. Mungu amemfanikisha baba yangu naamini ni kwa sababu tu alipatia eneo la kuishi, naamini kama angeishi Tukuyu wala asingelikuwa na mafanikio aliyo nayo sasa, yawe ya kiroho au kiuchumi, hata kiafya. Ngoja nikupe mfano huu wangu mwenyewe, sikia. Mimi sikupanga kuishi Mbeya, kama kuna sehemu niliyokuwa siipendi hata kutembelea ni Mbeya, Mungu alisema na mimi kuwa natakiwa nihame nilipo kuwepo na nihamie Mbeya. Siku ile Mungu anasema nami nilipata tabu sana kuupokea ujumbe huo kutoka kwa Mungu.Nilipokubali kuhama katika eneo nililokua naishi kwa muda wa miaka mingi, nimemuona Mungu akinifanikisha hatua kwa hatua. Mungu aliniambia kuwa amepanga niishi Mbeya.

Ngoja nikupe mfano huu mwingine uone na uelewe. Mimi ni mfanyakazi nimeajiriwa, unajua siku moja nilipokea ombi toka kwa Mkurugenzi wangu mkuu, akiniambia nihamie Arusha kikazi, Arusha ndio makao yetu makuu ya shirika katika Afrika, sikia, miezi miwili kabla sijapokea ombi hilo toka kwa Mkurugenzi wangu, Mungu alisema nami, alinionyesha nahama Mbeya, nina kwenda Arusha, baada ya kunionyesha safari yangu nzima ya kuhamia Arusha, akamalizia kwa kusema nami. Akaniambia kuwa nisihame Mbeya, akaniambia yeye anataka nikae Mbeya wala si Arusha. Nikamshirikisha mke wangu ujumbe huo, na tukatulia kusubiri kuona nini kitatokea. Baada ya ya miezi miwili ndio nikapewa taarifa ya kuhamia Arusha tena tukiwa mimi na mke wangu. Kilicho tusaidia ni kuwa tayari tulijua kuwa mpango wa Mungu ni nini, tukaamua kuongea na Mungu atupe hekima ya kuongea na Mkurugenzi .

Unajua nilikataa kuhamia Arusha, kwa kweli kibinadamu ilikuwa ngumu sana, kwani huko ambako ningehamia kulikuwa na kazi kubwa ya kuvutia. Kuna magari mazuri ambayo ningeyatumia, pia ningekuwa nafanya kazi makao makuu ya shirika. Unajua kilichonisaidia ni kwa sababu Bwana aliniambia mapema juu ya mahali anapotaka nikae alipanga nikae Mbeya,Baada ya hayo Mungu aliniambia mpango wake kwangu wa kuniweka Mbeya ni nini, aliniambia habari za utumishi aliouweka ndani yangu mimi na mke wangu, akasema wazi ili utumishi huo uchanue lazima nikae Mbeya. Nilishangaa sana, kwani Mbeya ni eneo ambalo kibinadamu ni gumu sana kuinuka kiutumishi kutokana na mazingira ya Mbeya na mapokeo yaliyopo Mbeya, hata hali ya kiuchumi tu Mbeya panaonekana ni pagumu sana.

Watu wa Mbeya hawana elimu toshelevu ya kutoa sadaka nk. Baada ya kumtii Mungu tu, kweli kile alichoniambia nimeanza kukiona, katika habari za utumishi, na hata kiafya na kiuchumi pia. Sio kama nataka kujisifu la hasha, nataka nikuonyeshe kitu katika sehemu hii ya eneo la kuishi jinsi lilivyo muhimu sana. Nataka wewe ndugu yangu ujiulize swali hili ni watu wangapi hawaishi pale Mungu alitaka waishi kisa eti wamepandishwa cheo? Au huko waendako kuna mshahara mnono nk.

Ukiyasoma maneno ya Mungu katika kitabu cha **Mathayo y**anasema hivi.

"Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake amemweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amini, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."
(Mathayo 24:45-51)

Ukiyasoma maneno hayo ya Mungu utaona wazi kuwa Bwana Yesu alikuwa anatoa mfano huo wenye fundisho kubwa kwetu la kujua umuhimu wa sisi kukaa mahali pale Mungu anataka tukae. Katika maneno hayo utaona wazi kuwa iwapo mtu akakosea mahali pa kuishi kuna hatari ya kukatwa na kutupwa au kupelekwa katika mahali penye kilio au msiba.

Ukiwaangalia watoto wa Mungu wengi leo hii wanaishi maisha ya kilio au majuto sana, hawajui ni kwanini. Sikiliza Mungu amekuandalia eneo ambalo anataka uishi hapo, anachotafuta kwako ni wewe kulijua eneo hilo, kama huna ufahamu au akili nakuambia ukweli utaishi eneo ambalo hakukupangia ukae. Sikiliza jiwekee utaratibu wa kuomba kuhusu jambo hili la kuishi kwako mahali pale Mungu atakapo uishi. Hebu tusonge mbele kidogo.

KUTAFUTA UNAFUU WA MAISHA (KIAKILI)

Bahati mbaya sana watoto wa Mungu wengi sana wanakaa mahali au wanaenda kuishi sehemu fulani kisa wanasema wanatafuta maisha huko wanakokwenda. Sikiliza kama unaishi eneo fulani na huko kuna ugumu wa maisha na unataka au unafikiri ulihame eneo hilo nakushauri kabla haujaamua wapi uende ukaishi tafuta kwanza ushauri kwa Mungu. Mungu yupo tayari kukushauri nakukuongoza katika njia unayotakiwa upite. Usiogope kumuuliza Mungu ni wapi amekupangia uishi. Mungu ametupa nafasi ya kumuuliza maswali mengi, au ametupa nafasi ya kumuomba ushauri, Angalia maneno yake yasemavyo.

"Bwana, Mtakatifu wa Israeli, na Muumba wake, asema hivi; Niulize habari za mambo yatakayokuja; mambo ya wana wangu, na habari ya kazi ya mikono yake; haya niagizeni"
(Isaya 45:11)

Muulize habari za kuishi kwako hapa duniani ni wapi anataka uishi, mwagize akuambie, nakuambia ukweli atakuambia na atakushauri.

Ona tena maneno haya ya Bwana yasemavyo**.**

"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; nitakushauri, jicho langu likikutazama".
(ZABURI 31:8-9)

Mungu yupo tayari kukufundisha na kukushauri, itategemea jinsi wewe mwenyewe umejipangaje. Angalia mfano huu, Yakobo alipokuwa amekaa Kanani na njaa kali ilipoivamia Kanani neno la Mungu linasema Mungu yeye ndiye aliyempa ushauri Yakobo wa kuhamia Misri. Angalia maneno haya ya Bwana yasemavyo

"Akasafiri Israeli, pamoja na yote aliyokuwa nayo, akaja Beer-sheba, akamchinjia sadaka Mungu wa Isaka na babaye. Mungu akanena na Israeli katika ndoto ya usiku, akasema, Yakobo, Yakobo akasema, mimi hapa. Akasema, Mimi ni Mungu, Mungu wa baba yako, usiogope kushuka mpaka Misri; maana nitakufanya uwe taifa kubwa huko, mimi nitashuka pamoja nawe mpaka Misri, nami nitakupandisha tena bila shaka; na Yusufu ataweka mkono wake juu ya macho yako."
(MWA 46:1-4).

Mungu ndiye aliyemwambia Yakobo aondoke Kanani aende Misri, kisa kulikuwa na njaa kali sana katika nchi ya Kanani.

Ona mfano huu mwingine. Isaka alikutana na hali ngumu ya njaa katika eneo alilokuwa anaishi, hakuondoka katika eneo hilo bila muongozo kutoka kwa Mungu, sikiliza maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Ikawa njaa katika nchi hiyo, mbali na njaa ile ya kwanza iliyokuwako siku za Ibrahimu. Isaka akamwendea Abimeleki, Mfalme wa Wafilisti, huko Gerari. Bwana akamtokea, akasema, usishuke kwenda Misri, kaa katika nchi nitakayokuambia. Kaa ugenini katika nchi hiyo, nami nitakuwa pamoja nawe, na kukubariki, maana nitakupa wewe na uzao wako nchi hizi zote. Nami nitakifanya imara kiapo nilichomuapia Ibrahimu baba yako."
(MWANZO 26:1-3)

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi kuwa Mungu anahusika sana na eneo unalopaswa uishi. Isaka alikatazwa na Mungu asiende Misri, bali aende Gerari, akae hapo, na Mungu akamwambia wazi kuwa akifanya hivyo ndipo atakapo pokea baraka kutoka kwa Mungu. Hebu nikuulize swali, kama Isaka angeenda Misri je! Mungu angembariki? Na angekuwa pamoja naye? niaminivyo mimi ni kuwa kama Isaka angeenda Misri asinge pokea baraka kutoka kwa Mungu, na Mungu asingekuwa pamoja na Isaka. Wewe angalia maneno hayo kwa makini utaona jinsi yalivyojaa maonyo kutoka kwa Bwana. Alimwambia wazi kuwa kama ataenda katika nchi atakayomwambia hapo ndipo atakapo mbarikia na kuwa pamoja naye. Naamini Isaka asingemtii Mungu, Isaka angepoteza baraka zake zote alizoahidiwa na Mungu. Wakristo wengi hawana muda wa kutafuta muongozo kutoka kwa Mungu kwa ajili ya jambo hili la mahali pakuishi, wengi wanaishi maeneo ambayo Mungu hakuwaambia waishi matokeo yake wanajikuta wapo kwenye taabu nyingi sana.

Hebu leo hii fuatilia uone utagundua hiki ninacho kuambia, watu wengi wanahamia maeneo fulani bila muongozo wa Mungu, wanayakimbia maeneo wanayoishi kwa sababu ya njaa iliyopo katika maeneo hayo,kuondoka si dhambi, ninachotaka ujifunze ni hiki, usiondoke katika eneo hilo bila ushauri kutoka kwa Mungu. Kwani hujui huko unakokimbilia kuna hatari gani, ona mfano huu uliomo ndani ya Biblia. Alikuwepo ndugu mmoja jina lake ni Elimeleki, yeye aliikimbia njaa katika eneo alilokuwa anaishi,

aliondoka na kwenda nchi ya Moabu. Matokeo yake yeye alikufa, na watoto wake wawili wa kiume walikufa, kisa, hakumuuliza Mungu aende wapi baada ya eneo alilokuwa akiishi kuwa gumu kwa njaa. Sikiliza maneno haya yanavyo sema.

"Ikawa zamani za Waamuzi walipoamua, kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Bethlehemu ya Yuda, akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye mkewe na wanawe wawili. Na jina la mtu huyo aliitwa Elimeleki, na jina la mkewe Naomi, na majina ya wanawe wawili Maloni na kilioni, Waefrathi wa Bethlehemu ya Yuda. Wakafika nchi ya Moabu, wakakaa huko. Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; na yule mwanamke akasalia na wanawe wawili. Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la mmoja aliitwa Orpa, na jina la pili Ruthu.wakakaa huko yapata miaka kumi. Wakafa Maloni na kilioni wote wawili; na huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili na mumewe pia."
(RUTHU 1:1-5).

Hao watu walikuwa na matatizo yanayofanana. Yakobo alikuwa na tatizo la njaa kali katika nchi aliyokuwa anaishi, na Elimeleki pia alikuwa na tatizo la njaa katika nchi anayoiishi. Ukiangalia Yakobo, alipewa ushauri na Mungu wa kuondoka katika nchi aliyokuwa anaiishi na Elimeleki yeye hakuambiwa na Mungu aende Moabu, alijiendea kwa kutumia akili zake, matokeo yake yalikuwa ni yeye kupoteza uhai wake na kwa watoto wake pia. Nakushauri mpendwa hakikisha haujitafutii unafuu wa maisha kwa kujiendea kuishi katika mji ambao huna uhakika kuwa Mungu anataka uishi hapo. Yasije kukuta mambo kama haya ya Elimeleki na wanawe.

MFANO WA MJI IUAYO WATUMISHI

Nataka hapo niseme kwa tahadhari kubwa. Si kila mji unapaswa kuishi, ukisoma neno la Mungu utagundua wazi kuwa ipo miji ambayo imetajwa kuwa miji hiyo inaua watumishi. Ona maneno haya ya Bwana Yesu mwenyewe akiuzungumzia mji wa Yerusalemu anauambia hivi.

"Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe waliotumwa kwako, mara ngapi nimetaka kuwakusanya watoto wako kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, wala hamkutaka."
(LUKA 13:34).

Ukiyaangalia maneno hayo utagundua kuwa Mji huo ndio uliokuwa chimbuko la kuwaua hao watumishi wa Mungu, sikiliza ipo miji mingine inatabia hiyo, inaua watumishi, isipowaua kiroho inawaua kimwili, au inawaua kihuduma. Wewe fuatilia utaona, kuna sehemu watumishi wakihamia tu, huduma zao zinakufa kabisa, au wanakufa kimwili mapema, Ukifuatilia utaona ipo miji mingine neno la Mungu linaitaja wazi kuwa inazuia watu kuokoka.

Ona mfano wa miji hii, ambayo Yesu aliita miji isiyo tubu, hasemi watu anasema miji!

"Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza yake iliyo mingi, kwa sababu haikutubu. Ole wako Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika tiro na sidoni,wangelitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu, walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi.
(MATHAYO 11:20-22).

Fahamu ukiishi katika mji huo ni vigumu kuokoka hata ifanyike miujiza ya aina gani, au hata uhubiriwe injili na mtumishi mwenye kiwango cha juu kwa kuwa tu, unaishi kwenye mji wa namna hiyo fahamu huwezi kuokoka, bahati mbaya watu wengi hawalijui jambo hili, wengi wanasema kama kuhubiriwa tunahubiriwa kweli ila hatubadiliki au watu hawaokoki, unajua sababu nini? Inawezekana ni kwa sababu ya mji huo unao ishi!

Ikiwa muujiza kama huo utafanyika katika mji mwingine fahamu watu hao hao wakienda katika mji huo mwingine wataokoka. Sikia Yesu anaitaja miji ya Tiro na Sidoni kuwa injili ile iliyo hubiriwa huko Korazini na Bethsaida kama ingehubiriwa katika miji hiyo ingetubu hiyo miji ya Tiro na Sidoni. Sikiliza kuna miji inazuia wokovu, kuna miji inawaua watumishi, kuna miji inafilisi watoto wa Mungu nk. Kwa hiyo inatakiwa uwe makini sana hebu fikiri unaishi kwenye mji wenye sifa za namna hii

"Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu: kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe."
(MATHAYO 11:23-24).

Hebu fikiri wewe unaishi kwenye mji wa namna hiyo, ambao Bwana anausemea maneno magumu namna hiyo, siku akiamua kuupeleka mji huo kwenye maangamizo na wewe unaishi kwenye mji huo unafikiri utapona? Kamuulize Lutu, alibahatika tu, lakini cha moto alikiona alipokosea kuishi Sodoma na Gomora. Angalia leo hii ukisikia kuna vita kati ya nchi fulani na nchi fulani kuna miji ambayo inaharibiwa vibaya sana, cha ajabu utaona miji mingine inasalimika kabisa utafikiri vita haikupiganwa katika nchi hiyo na katika mji huo. Umewahi jiulize ni kwa nini? Sikiliza kila mji unahukumu zake, na hukumu hizo zinatokea kabla hata Yesu kuja mara ya pili. Wewe ufuatilie mji wa Yerusalemu utaona Yesu aliutabiria kuwa utaangamia, ni kweli. Mji huo ulikuja bomolewa vibaya sana. Hata miji ya Iraki ili tabiriwa kuja kupigwa vibaya sana na mataifa kutoka mbali, fahamu Iraki ndiyo Babeli. Soma kitabu cha **(ISAYA 13:1-22).** Pia yaangalie maneno haya ya Bwana yakisema juu ya Babeli au Iraki ya sasa

"Kimbieni kutoka Babeli, mkatoke katika nchi ya Wakaldayo, mkawe kama mabeberu

mbele ya makundi. Kwa maana juu ya Babeli nitaamsha na kuleta kusanyiko la mataifa makubwa, toka nchi ya kaskazini; nao watajipanga juu yake; kutoka huko atatwaliwa; mishale yao itakuwa kama ya mtu shujaa aliye stadi; hapana hata mmoja utakaorudi bure. Nao Ukaldayo utakuwa mateka; wote wautekao watashiba, asema Bwana."
(YEREMIA 50: 8-10).

Fikiri sasa wewe ndio umeenda kichwa-kichwa kuishi kwenye miji ya namna hiyo hujui Mungu kainenea nini, nakuambia ukweli utapata shida siku miji hiyo ikiharibiwa. Swali langu kwako ni hili ni nani kakuaambia uishi kwenye mji huo? Anza kuomba ili Mungu akuongoze kwenye mji aliokupangia.

Hebu tusonge mbele, tuone faida ya kukaa mahali Mungu anataka uishi.

FAIDA YA KUISHI MAHALI AU ENEO MUNGU ANATAKA UISHI

Ukiyasoma maandiko matakatifu kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu utaona wazi kuwa ikiwa utaishi eneo lile Mungu atakalo uishi fahamu kuna faida sana utazozipata. Hebu tuone faida ya kwanza nayo ni.

KUOKOLEWA NA ADUI ZAKO

Watu wengi sana wanatafuta ulinzi kwa Mungu. Wengi wanaomba sana Mungu awaokoe na mambo mbalimbali mabaya. Moja ya jambo ambalo Mungu anaweza kulitumia ili akuokoe na adui shetani ni hili la kukaa katika mji autakao yeye ukae. Atakupeleka ukaishi eneo fulani. Angalia mfano huu mzuri utaelewa ninacho kisema. Siku ile Yesu anazaliwa shetani alitafuta kumuua. Neno la Bwana linasema Mungu, alimuokoa Yesu, na alitumia nchi(eneo) ili kumuokoa. Angalia maneno haya yasemavyo.

"Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume. Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani, hata mahali pake, hapo alishwapo kwa wakati na nyakati na nusu ya wakati, mbali na nyoka huyo. Nyoka akatoa katika kinywa chake. Nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto, amfanye kuchukuliwa na mto ule. Nchi ikamsaidia mwanamke; nchi ikafunua kinywa chake, ikaumeza mto ule alioutoa yule joka katika kinywa chake. Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari"
(UFU 12:13-17).

Ninaamini kuwa unajua sana habari za Bwana Yesu kutafutwa kuuwawa akiwa bado ni mtoto mdogo, ila inawezekana ulikua hujui ni mambo gani yaliyokuwa yakitendeka katika ulimwengu wa roho. Ukiyasoma maneno hayo hapo juu utaona wazi kuwa Mungu

alimwokoa mama na mtoto kwa kutumia nchi au eneo. Mungu alitafuta eneo ambalo nyoka alishindwa kufika huko. Katika ulimwengu wa mwili ilikua hivi, siku Bwana Yesu anazaliwa, mfalme Herode alipopata habari alitafuta kumuua Yesu. Kwa maana nyingine mfalme Herode alikuwa ni joka! Ona maneno haya yasemavyo.

"Na hao walipokwisha kwenda zao malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto akasema, ondoka umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hatanikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize. Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda Misri; akakaa huko hata alipokufa Herode; ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, kutoka Misri nalimwita mwanangu....."
(MATHAYO 2:13-15).

Herode alikuwa joka ambaye alikusudia kumuua Yesu alipozaliwa. Mungu aliitumia nchi au eneo la Misri kumuokoa Yesu na mama yake, ukiona hapo utagundua Mungu alitumia nchi ya Misri kama ukombozi kwa Yesu na mama yake, hata alipo kufa Herode bado Mungu alilitumia eneo kama sehemu ya ulinzi kwa Yesu Kristo. Alipokufa Herode Mungu alimwongoza Yusufu sehemu ya kwenda na mtoto. Angalia maneno haya ya Bwana yasemavyo

"Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, akasema, ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto. Akaondoka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli. Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Uyahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya, akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, ataitwa Mnazorayo."
(MATHAYO 2:19-23).

Mungu anaweza hata leo hii kufanya hivihivi. Anaweza kulitumia eneo kama sehemu ya ulinzi wako wewe, watoto wa Mungu wengi hawalijui jambo hili ndio maana hawako makini katika kuomba kwao kuhusu jambo hili la eneo wanalotakiwa kuiishi. Wengi wanasema Mungu atanilinda, ila hawajui mfumo wa ulinzi wa kimungu ulivyo. Mungu anaweza kukulinda wewe kwa kutumia eneo. Akikuambia ondoka katika eneo hilo unaloishi, nakushauri ondoka, usiseme Bwana atanilinda hapahapa siwezi kuondoka. Hebu pata ufahamu huu. Yesu Kristo ni Mungu.

Kwanini Mungu asimlinde palepale alipokuwepo?Ilimlazimu aondoke eneo lile ndipo wokovu wake ungetokea. Sikiliza watoto wa Mungu wengi leo hii adui yao amewameza kisa wamekosea eneo la kuishi. Kama wakiondoka katika eneo wanaloishi na kwenda eneo ambalo Mungu anataka waishi ndipo usalama wao utakapotokea. Sikiliza, lazima leo ufahamu kuwa Mungu anapokuondoa eneo fulani na kukupeleka eneo lingine

inawezekana anataka alitumie eneo hilo kama sehemu ya ulinzi wako wewe, uwe wa rohoni au wa afya yako, kiutumishi nk.

Kuna watu wengine wakienda kusalimia nyumbani kwao tu, ndipo mabaya huwatokea, yawe magonjwa, vifo nk. Sikiliza kabla haujaenda huko kwenu kusalimia ndugu, au kwenye misiba, jifunze kutafuta muongozo kutoka kwa Mungu, muulize Mungu. Ukiona kuna amani ya kwenda nenda, kama hakuna amani nakushauri usiende. Hujui ni kwanini Mungu alikutoa huko kwenu na kukupeleka huko uliko sasa. Huenda Herode wako hajafa bado, subiri mpendwa, akifa Herode wako ndipo uwe huru kwenda huko unanisikia?.

Maeneo kama hayo yaliyojaa hatari Mungu anaweza kukupa neno la maarifa ya namna ya kuyaingia, ona mfano huu wa jinsi Yesu Kristo alivyokuwa makini katika kuishi kwake hapa duniani, si kila eneo lilikuwa na usalama kwake. Neno la Bwana linasema Yesu hakwenda katika maeneo mengine waziwazi, alikuwa anakwenda kwa siri. Ona maneno haya yanavyotufundisha.

"Na baada ya hayo Yesu alikuwa akitembea katika Galilaya; maana hakutaka kutembea katika Uyahudi, kwa sababu Wayahudi walikuwa wakitafuta kumwua. Na sikukuu ya Wayahudi, siku ya Vibanda, ilikuwa karibu. Basi ndugu zake wakamwambia, ondoka hapa, uende Uyahudi, wanafunzi wako nao wapate kuzitazama kazi zako unazozifanya. Kwa maana hakuna mtu afanyaye neno kwa siri, naye mwenyewe ataka kujulikana. Ukifanya haya basi jidhihirishe kwa ulimwengu. Maana hata nduguze hawakumwamini. Basi Yesu akawaambia, haujafika bado wakati wangu;ila wakati wenu siku zote upo. Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu. Kweeni ninyi kwenda kula sikukuu; mimi sikwei bado kwenda kula sikukuu hii; kwa kuwa haujatimia wakati wangu. Naye alipokwisha kuwaambia hayo, alikaa vivi hivi huko Galilaya. Hata ndugu zake walipokwisha kukwea kuiendea sikukuu, ndipo yeye naye alipokwea, si kwa wazi bali kana kwamba kwa siri."
(YOHANA 7:1-10).

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi jinsi eneo la Galilaya lilivyokuwa ni sehemu ya ulinzi kwa Bwana Yesu Kristo. Hakuenda Uyahudini kwa sababu adui yake alikuwako huko. Akakaa Galilaya kwa amani, hebu fikiri sana huyo Yesu ni Mungu, kwanini asiende kila eneo ovyo ovyo? Fikiri kwanini aende Uyahudini kwa siri yaani kwa kujificha? Ukiyaangalia maneno hayo kwa makini utakiona ninacho kuambia kuwa ukipatia kukaa katika eneo ambalo Mungu anataka ukae, unapata ulinzi dhidi ya maadui zako. Tatizo kubwa lililopo kwa watoto wengi wa Mungu ni hili, tumeokoka kupitia msalaba! Tunaweza kwenda eneo lolote lile huku tukijiamini sana kuwa pale naenda adui hawezi kunifanya kitu! Matokeo yake ni kupigwa au kushindwa. Na hapo ndipo wengi hufikiri mambo mengi yasiyofaa. Yesu alijua eneo analotakiwa akae ili adui asimwangamize,

kumbuka, huyo ni Yesu Kristo Mfalme. Alijua kabisa kuwa eneo la Galilaya ndilo lenye usalama kwake hakutoka ovyoovyo katika eneo hilo. Hata alipotoka hakutoka kichwa-kichwa, alitoka kwa siri. Je! Ungekuwa ni wewe ungefanya nini?

Sikiliza mpendwa, inatakiwa uwe makini sana katika suala hili, usiishi kila eneo bila muongozo wa kutoka kwa Mungu. Hata kama umepata uamisho kikazi usikurupuke kukataa, au kuukubaria bila kutafuta muongozo kutoka kwa Mungu. Mungu anaweza akawa leo hii anakuokoa na adui yako aliyeko huko nyumbani kwenu, ndio maana unamuomba sana akusaidie uhame katika eneo hilo unaloishi ili uende kwenu lakini mpaka sasa haujafanikiwa. Tulia, muulize Mungu ni kwanini upo hapo, na unapomuomba akuhamishe amekaa kimya. Atakuambia kwanini hajakuamisha. Hebu tuangalie faida ya pili, nayo ni.

FAIDA YA PILI MUNGU KUJIFUNUA KWAKO KWA URAHISI

Ili leo hii Mungu apate kujifunua kwako na mawasilianao yako na Mungu yawe mazuri, lazima ujue kuwa itategemea eneo unaloishi. Ngoja nikupe mifano hii, Baba Mungu alimweka Adamu bustanini Edeni, Mungu alikuwa akimtembelea Adamu pale bustanini. Adamu alipokula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya alienda eneo lingine kujificha. Mungu alipotaka kuwasiliana na Adamu hakwenda katika eneo lile ambalo Adamu alikuwa amejificha. Alienda pale alipomuweka. Si kwamba Mungu alikuwa hajui kuwa Adamu hayupo pale alipomweka aishi, Mungu alijua kabisa kuwa Adamu hayupo pale, pia si kuwa Mungu alishindwa kwenda sehemu ile ambayo Adamu kajificha, alikuwa na uwezo kabisa wa kwenda pale alipojificha Adamu, Mungu alienda eneo lile alilomuweka Adamu aishi, alipomkosa ndipo alipomwita Adamu uko wapi. Swali ni hili, kwa nini Mungu alienda pale alipomuweka Adamu ? kwa nini hakwenda eneo lile Adamu alipojificha?

Angalia haya maneno ya Bwana yasemavyo “Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, uko wapi? Akasema nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.” (MWANZO 3:8-10). Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Mungu ili awasiliane na mtu huwa anaheshimu sana eneo lile alilomuweka huyo mtu aishi. Kumbuka Mungu alijua kabisa kuwa Adamu hayupo pale alipomuweka, hakwenda kule Adamu alikojificha alienda moja kwamoja eneo lile alilomuweka Adamu aishi.

Watu wengi leo hii, wamejikuta hawana mawasiliano mazuri na Mungu, hawawezi kuomba tena kama zamani, hawana maono kama zamani, Mungu hasemi nao kama zamani. Neno la Mungu linasema upo uwezekano kabisa wa kupoteza mawasiliano kabisa na Mungu, ona neno la Mungu lisemavyo.

"Basi, mtoto Samweli akamtumikia Bwana mbele ya Eli. Na neno la Bwana lilikuwa adimu siku zile; hapakuwa na mafunuo dhahiri."
(1SAMWELI 3:1).

Ukiyaangalia maneno hayo utagundua kuwa upo uwezekano wa mtu kupoteza mawasiliano mazuri na Mungu. Na moja ya jambo linaloweza kukupotezea mawasiliano yako mazuri na Mungu ni hili la kukosea eneo ambalo Mungu alitaka ukae. Wakristo wengi mawasiliano yao na Mungu yanapokatika wanaangaika sana kutafuta ni wapi mawasilianao yao yalipo katikia. Sikiliza fuatilia katika kona hii ya eneo unaloishi, linaweza likawa ndio chanzo cha wewe kupoteza mawasiliano na Mungu.

Si kila eneo kuna urahisi wa wewe kuwa na mawasiliano mazuri na Mungu, maeneo mengine ni magumu sana. Maeneo mengine Biblia inasema ni langa la mbinguni, ona maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani. Akafika mahali ulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake. Akalala usingizi pale pale. Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamisha juu ya nchi na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake. Na tazama Bwana amesimama juu yake, akasema, mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka;... ."(MWANZO 28:10-13) Angalia mistari hii pia. "Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, kweli Bwana yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. Naye aliogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka,hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo langa la mbinguni."
(MWANZO 28: 16-17).

Sikiliza Yakobo anasema mahali hapo ni nyumba ya Mungu. Ni langa la mbinguni, kumbe basi ukipatia eneo la kuishi ambalo Mungu anataka uishi, unakuwa unaingia kwenye nyumba ya Mungu au unakuwa kwenye langa la mbinguni. Mawasiliano yako na Mungu yanakuwa si ya kawaida, Mungu atajifunua waziwazi kwako, kwa sababu upo nyumbani kwake au mlangoni kwake, wewe fikiria mtu anaye ishi ndani ya nyumba yako jinsi anavyoweza kukuona waziwazi kuliko yule aliye mbali na nyumba hiyo unayoishi. Maeneo mengine yote Yakobo hakuwahi kumuona Bwana. alipofika eneo hilo ndipo alipomuona Bwana, yaani Bwana alijifunua kwa Yakobo.

Fahamu kuna maeneo mengine ni langa la mbinguni,eneo hilo linapitisha kirahisi vitu vya mbinguni. Ukikaa kwenye eneo hilo ni rahisi sana kuwa na mwasiliano kirahisi na Mungu. Pia maeneo ya namna hiyo ni rahisi sana Mungu kujifunua kwako. Mungu anapokuongoza uende kuishi eneo fulani fahamu moja ya faida ya hilo eneo ni kuwa na mawasiliano kati ya wewe na Mungu. Mungu akikuambia uishi eneo fulani anajua kabisa kuwa eneo hilo analokutuma lazima litapitisha vitu vya mbinguni kirahisi, ona Yakobo

alipofika kwenye eneo lile yeye mwenyewe anakiri kuwa aliona malaika wanapanda na kushuka, pia aliisikia vizuri sauti ya Mungu, swali langu ni hili, Yakobo alilala kwenye maeneo mangapi kabla ya kulala hapo alipolala na kuyaona hayo aliyoyaona? Jibu ni kuwa alilala katika maeneo mengi tu, lakini hakuwahi kuyaona hayo aliyoyaona katika eneo la Betheli. Najaribu kukupa mifano hiyo ili ujue kuwa si kila eneo utayaona mambo ya Mungu kwa urahisi.

Kama kuna maeneo Biblia inasema ni mlango wa mbinguni, basi lazima kuna maeneo ambayo ni milango ya kuzimu. Yaani maeneo hayo yanapitisha kirahisi mambo ya kuzimu. Nakumbuka kuna eneo fulani nilikwenda kufanya huduma, Mungu alinipa kibali cha kwenda huko, sitaisahau huduma ile katika maisha yangu, kwani eneo lile lilikuwa gumu kwelikweli, nakumbuka kabla sijaenda eneo lile, nilifanya maombi kwa muda mrefu kidogo juu ya huduma hiyo, unajua siku moja niliona maono juu ya huduma hiyo, niliona shetani akinitisha kuwa nimemfuata kwenye eneo ambalo hakutaka niende. Alisema wazi kuwa ' YAANI UNANIFUTA HATA HUKU? Sikiliza niliona jinsi vita itakavyokuwa, Bwana alinipigania, nikaenda huko. Na ninakuambia ukweli nilipokwenda kwenye huduma ile nilikutana na vita kubwa sana, namshukuru Mungu alinipigania sana. Nilipofika kule niliona kitu ninachokuambia wazi wazi hakukuwa na uhuru mkubwa wa kuwasiliana na Mungu kwa njia ya maombi kama maeneo mengine. Anga lile lilikamatwa na shetani, ardhi pia ilikamatwa na shetani, ilikuwa ni vita ya kubomoa ngome ya adui, nina amini eneo lile lilikuwa ni lango la shetani likipitisha mambo mengi ya adui.

Wewe mwenyewe jaribu kuvuta kumbukumbu zako, utaona kuna maeneo ulipoenda hata kuomba ulikuwa huwezi kabisa, ukitaka kusoma neno la Mungu huwezi kabisa, hata ukisoma hukielewi kabisa ukisomacho, yaani unajikuta unataka kuomba lakini maombi yako yanakurudia hayaendi, fahamu eneo hilo ulilopo ni lango la shetani. Kama Mungu hajakupa kibali cha wewe kuwepo hapo nakuambia ukweli una muda mfupi sana wa kusimama katika imani. Utaanguka tu. Kwaninini nasema hivyo sikiliza huna mawasilino na Mungu wako, huwezi hata kumuita au kumsikiliza unakuwa kama upo kisiwani.Kama huna msaada toka mbinguni,unafikiri utaishindaje hiyo vita? Si utapigwa tu.

Hata nyumba hizi tunazoishi za kupanga, sikiliza, kuna nyumba ukiingia tu, maombi yako yote yanakatika. Huwezi kusoma neno la Mungu kama zamani hata ukisoma wala huelewi, ukitoka tu hapo ndani unaona kiu ya maombi inakuja, unasoma neno linaeleweka, ukirudi hapo nyumbani shida ni ileile. Sikiliza ukiona hivyo fahamu nyumba hiyo kuna lango la adui, ukiona hivyo nakushauri, fanya maombi maalum, au tafuta nyumba nyingine ya kupanga, tena muombe Mungu akuongoze ni nyumba ipi unatakiwa ukapange na uishi hapo. Si kila nyumba ni nzuri kwa kuishi wewe mtoto wa Mungu hata kama ni ya kupendeza sana, wewe hujui hapo ni lango la nani, ni la mbinguni au la kuzimu. Yakobo anasema wazi hakujua, alijilalia tu kwenye eneo hilo

baadaye ndipo anagundua kuwa eneo hilo ni nyumba ya Mungu na ni lango la mbinguni. Je! Wewe umegundua hapo unapolala au unapoishi ni lango la wapi?

Kuna maeneo mengine watu hawana hofu ya Mungu kabisa, maeneo ya namna hiyo asilimia kubwa yanapitisha sana mambo ya adui, ukiwa katika maeneo hayo utajikuta unakuwa mkavu sana kiroho. Yaani mawasiliano yako na Bwana Yesu hayawi mazuri, yapo maeneo ya namna hiyo. Ona mfano huu wa eneo kama hilo.

"Ibrahimu akasema, kwa sababu naliona, yakini hapana hofu ya Mungu mahali hapa……."
(MWANZO 20:11).

Ibrahimu aligundua jambo hilo alipofika na kuishi kwenye eneo hilo, alimwambia Mfalme Abimeleki kuwa aliamua kusema Sara ni dada yake wala si mke wake kwa sababu mahali hapo hapakuwa na hofu ya Mungu. Sikiliza, anasema **"MAHALI HAPA".** Hasemi watu hawa hawana hofu ya Mungu. Anasema mahali hapa. Neno mahali hapa maana yake alilizungumzia eneo, eneo hilo lilikuwa halina hofu ya Mungu, kumbe basi kuna maeneo yana hofu ya Mungu. Kama eneo hilo lina hofu ya Mungu hata watu wa eneo hilo watakuwa na hofu ya Mungu, kumbuka hili ninalokuambia katika maisha yako yote. Ukilijua jambo hilo hata maombi yako utayabadilisha utaliombea eneo hilo unaloishi liwe na hofu ya Mungu. Kwa kuwa hatujui ndio maana hukuti maombi kama hayo kwa watoto wengi wa Mungu.

Eneo lenye hofu ya Mungu linakuwa ni eneo zuri sana hata kwa Mungu kujifunua kwako. Ngoja nikupe mfano huu wa mwisho halafu tuone faida nyingine. Wakati ule Bwana Yesu Kristo amefufuka, aliwaagiza wanafunzi wake waende Galilaya, alisema huko ndiko watakakomuona, sikiliza maneno haya yasemavyo.

"Kisha Yesu akawaambia, msiogope: enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona."
(MATHAYO 28:10)

Angalia na mistari hii mingine.

"Na wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu. Nao walimwona, wakamsujudia:..."
(MATHAYO 28: 16).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua wazi kuwa Bwana Yesu alilichagua eneo hilo la Galilaya ili ajifunue kwa wanafunzi baada ya kufufuka, swali kwanini hakulitafuta eneo la Yerusalemu? Au maeneo mengine? Kumbuka hao wanafunzi walikuwepo Yerusalemu. Alilichagua eneo hilo la Galilaya naamini aliliona ndilo eneo bora la kujifunua kwa

wanafunzi wake lilikuwa ni eneo ambalo mimi naliita lango la mbinguni lililotumika sana na Bwana Yesu kupitishia vitu vya mbinguni. Angalia tena, aliwaagiza hao wanafunzi waende kwenye mlima ambao aliuchagua. Fikiria tena, kwanini uwe mlima huo? Nataka utanuwe mawazo yako juu ya jambo hili ninalokufundisha, sikiliza si kila mlima nirahisi Bwana kujifunua kwako! Kuna eneo atakuchagulia uende,ukienda huko hapo ndipo itakuwa rahisi kwako kumuona,na kumsikiliza. Watu wengi hupenda kutafuta mlima na kwenda kuomba, sikiliza, usikurupuke kujitafutia kila mahali palipoinuka ukafikiri salama kwenda kuomba. Unaweza kwenda huko ukakutana na shetani badala ya Bwana Yesu uwe mwangalifu mpendwa.

Swali langu ni wapi Mungu amekuagiza ukaishi? Au amekupa kibali cha kuishi? Kama huna uhakika anza leo kumuomba juu ya jambo hilo. Ukijua na ukatii na ukaishi hapo, ni rahisi sana kwako kuwa na mawasiliano mazuri na Bwana, sina maana maeneo mengine hawezi kukusikia, ninachotaka ukione ni urahisi wa wewe kuwa na mawasiliano mazuri na Bwana. Fikiri Bwana aliwaagiza hao wanafunzi waende Galilaya, kama wangeenda mji mwingine kumsubiri aje kwao unafikiri Yesu angeenda huko? Hata kama angeenda unafikiri angeenda kwa furaha wakati analitaka na aliwaagiza hao ndugu waende Galilaya? hebu fikiri.

Watumishi wengi wamejikuta leo hii wamepoteza mawasiliano yao na Bwana na hawajui ni kwa nini Bwana hajifunui kwao kama zamani. Unajua moja ya sababu ambayo inaweza kuwa imepelekea tatizo hilo ni hili la mtumishi wa Mungu kutokuwepo mahali Mungu alitaka wawepo ona maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake?"
(MATHAYO 24: 45).

Ukiyaangalia maneno hayo utaona jambo ninalokuambia, Mungu hujishughulisha sana na maeneo. Anasema ni nani basi mtumwa yule mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake **alimweka**.... Neno alimweka maana yake anazungumzia sehemu au eneo fulani ambalo Bwana alikusudia huyo mtumishi wake awepo hapo.

Sasa fikiri mtumishi haupo hapo alipokuweka unafikiri huyo Bwana aliyekuweka hapo atakuwa na mawasiliano na wewe mazuri? Jibu ni rahisi sana hata kuwa na mawasiliano mazuri na wewe, kwa kuwa haupo pale alipokuweka. Mfano huyo Yesu aliutoa kwa ajili ya watumishi wake, akiwaonyesha namna anavyotaka watumishi wake wajue kuwa kuna mahali Mungu anataka wawepo, tena kwa wakati, kama wakiwepo hapo ninakuambia ukweli watumishi wa namna hiyo huwa kila mara Mungu hujifunua kwao na hata utumishi wao si wa kimazoea ni mpya kila siku, hawana jumbe zilezile za zamani, ni watumishi wenye mawasiliano mazuri na Bwana. Sikiliza mtumishi usiende kila sehemu iwe kwenye huduma au kuishi kwako bila kiballl,i kutoka kwa Mungu.

Mungu akisema nenda wewe nenda akisema usiende huko na kushauri usiende, kwani ukienda huko utapoteza mawasiliano naye. Na amini umenielewa katika sehemu hii ya faida ya pili. Hebu tusonge mbele tuone faida ya tatu. Nayo ni Kutunzwa na Mungu.

KUTUNZWA NA MUNGU

Mungu anatabia ya kutunza watoto wake, ona maneno haya ya Bwana wetu Yesu Kristo yasemavyo.

"Nilipokuwapo pamoja nao, mimi naliwalinda kwa jina lako ulilonipa, nikawatunza;..."
(YOHANA 17: 12).

Maneno hayo yanatufundisha kuwa, Mungu anatabia ya kutulinda na kututunza. Sikia, unaweza ukawa leo hii una maombi sana ya kutunzwa na Mungu, lakini unajikuta kwa kweli unaishi maisha magumu sana, kiasi ambacho huoni kama kweli Mungu anajishughulisha na habari za kutunzwa kwako. Ili Mungu akutunze wewe lazima ufahamu kuwa kutunzwa kwako kutaambatana na eneo unaloishi! Kama Mungu amekupeleka uishi eneo fulani ndipo wewe unapokuwa na uhalali wote wa kutunzwa na kupewa mahitaji yako yote na Mungu. Itakua ni rahisi kukupa mahitaji yako yote uyatakayo kwa sababu yeye ndiye amekuweka hapo, kinyume cha hapo usitegemee kupewa mahitaji yako kutoka kwa Mungu kama umekosea eneo la kuishi. Au niseme hivi, inakuwa ni ngumu kutunzwa na Mungu kwa kiwango kile alicho kupangia iwapo haupo mahali pale alipokuchagulia uishi.

Katika hili haijalishi wewe umeokoka au haujaokoka, ni mtumishi wa Mungu au si mtumishi wa Mungu, Mara nyingi nimekua na swali hili moyoni mwangu, kwanini watumishi wengi wa Mungu wanaishi maisha magumu sana Wakati Mungu ameahidi kuwatunza watumishi wake? Mungu ametuahidi akisema,

"Msiwe na tabia ya kupenda fedha: mwe radhi na vitu mlivyonavyo: kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. Hata twathubutu kusema Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa: Mwanadamu atanitenda nini?"
(EBR 13:5-6).

Mungu alipoanza kunifundisha kwa kupitia ujumbe huu alinipa mfano huu mzuri jinsi alivyowatunza watumishi wake.

Ona mfano huu mzuri, Eliya alitunzwa na Mungu ni kwa sababu alikuwepo eneo ambalo Mungu alitaka awepo, ona

"Neno la Bwana, likamjia, kusema ondoka hapa, geuka, uende upande wa mashariki, ujifiche karibu na kijito: nami nimewaamuru kunguru wakulishe huko. Basi akaenda

akafanya kama alivyosema Bwana: kwa kuwa akaenda akakaa karibu na kijito cha Kerithi, kinachokabili Yordani. Kunguru wakamletea mkate na nyama asubuhi, na mkate na nyama jioni, akanywa maji ya kile kijito. Ikawa, baada ya siku kupita kile kijito kikakauka, kwa sababu mvua haikunya katika nchi. Neno la Bwana likamjia, kusema, ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe."
(1FAL 17:2-9).

Baada ya kuyasoma maneno hayo hebu, jiulize swali hili, iwapo Eliya angekosea asingekuwepo mahali pale Mungu alitaka awepo je! Unafikiri kunguru angemtafuta sehemu nyingine? Kumbuka Mungu aliwaamuru kunguru waende kwenye kijito cha Kerithi, wapeleke chakula kwa Eliya tena kwa muda maalum, hebu fikiri, hao kunguru wameenda huko Kerithi wakamkosa Eliya, yeye kaenda kwenye kijito kingine au sehemu nyingine unafikiri hao kunguru wangeanza kuzunguka kumtafuta Eliya? Nakuambia ukweli wasinge mtafuta! Kama wangeliweza kumtafuta Mungu asingemwagiza Eliya ande kwenye kijito cha Kerithi, angemwagiza akae mahali popote na kunguru wangemtafuta huko. Sikiliza mpendwa leo hii ukipatia eneo la kuishi kwako unakua unajirahisishia kupokea kila kitu kutoka kwa watu ambao Mungu amewaamuru wakutunze.

Baadaye Mungu akamwagiza Eliya aondoke mahali hapo, akamwagiza aende Sarepta,

"Ikawa, baada ya siku kupita kile kijito kikakauka, kwa sababu mvua haikunya katika nchi. Neno la Bwana likamjia, kusema, ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe. Basi, akaondoka, akaenda Sarepta: hata alipofika langoni pa mji kumbe! Mwanamke mjane alikuwako akiokota kuni; akamwambia, niletee, nakuomba, maji kidogo chomboni nipate kunywa. Alipokuwa akienda kuleta, akamwita akasema, niletee nakuomba kipande cha mkate mkononi mwako. Naye akasema, kama Bwana, Mungu wako, aishivyo, sina mkate, ila konzi ya unga katika pipa, na mafuta kidogo katika chupa: nami ninaokota kuni mbili niingie nijipikie nafsi yangu na mwanangu , tuule tukafe. Eliya akamwambia, usiogope: enenda ukafanye kama ulivyosema; lakini unifanyie kwanza mkate mdogo ukaniletee; kisha ujifanyie nafsi yako na mwanao. Kwa kuwa Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi. Lile pipa la unga halitapunguka, wala ile chupa ya mafuta haitaisha hata siku ile Bwana atakapoleta mvua juu ya nchi. Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya na nyumba yake wakala siku nyingi. Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa kinywa cha Eliya"
(1FAL 17:7-16).

Mungu alimtunza Eliya kwa sababu alikwenda eneo lile Bwana alitaka Eliya awepo, fikiri kama Eliya asingelikwenda Sarepta je! Angekua na uhalali wa kutunzwa na

Mungu? Nakuambia ukweli asingelikua na uhalali wa kutunzwa na Mungu. Hata wewe ndugu yangu ikiwa leo hii utakosea kwenye eneo hili la kuishi fahamu unapoteza uhalali wa kutunzwa na Mungu. Ujasiri mkuu wa kumuomba Mungu atutunze tunaupata kama tutakuwepo mahali pale Mungu ametaka tuwepo. Tukiwepo hapo ni rahisi kumuambia atutunze kwa sababu yeye ndiye katuweka hapo. Mara nyingi watoto wa Mungu wengi wamejikuta wamekwama kwenye sehemu hii ya kupewa mahitaji yao na Bwana kwakuwa hawapo mahali pale Bwana alitaka wawepo. Ibrahimu alikua na ujasiri wote wa kumuomba Mungu amtunze kwa sababu Mungu ndiye aliye mtoa katika eneo alilokua anaishi, sehemu ambayo alikua na urithi wake pia alikua na jamaa zake, alipotolewa hapo na kupelekwa eneo lile Mungu anataka awepo, ndipo alipopata uhalali wa kutunzwa na Mungu katika eneo hilo, wewe fuatilia hata mazungumzo kati ya Mungu na Ibrahimu yalivyokua utaona kitu hiki ninacho kuambia, ona mfano huu

"Kisha akamwambia, mimi ni Bwana, niliyekuleta kutoka Uru wa Wakaldayo nikupe nchi hii ili uirithi"
(MWANZO 15:7).

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi kuwa Mungu anajieleza kwa Ibrahimu kuwa atampa hiyo nchi kwa sababu yeye Mungu ndiye aliye mleta Ibrahimu mahali hapo. Muulize Mungu swali hili, ikiwa Ibrahimu yeye mwenyewe amejipeleka mahali pale je! Mungu ungempa Ibrahimu nchi hiyo? Jibu atakalo kujibu ninalo amini mimi ni hili, asingempa baraka hizo. Ngoja nikupe mfano wa pili uone. Ukisoma kitabu cha Waamuzi sura ya kwanza yote utaona hapo kuna habari ya mtu anaeitwa Kalebu, Huyo Kalebu alikua na mtoto wa kike aitwae Aksa. Kalebu alimpeleka mtoto wake huyo wa kike kuolewa na mwanaume mmoja aitwaye Othnieli, huyo Aksa alikua na akili, alipopelekwa kwa huyo mwanaume, aligundua kuwa huyo mwanaume ahauhitaji wa mashamba nk, hakumpigia kelele mume wake, alijua kuwa mwenye wajibu wa kumpa hivyo vitu ni yule aliyempeleka huko ambaye alikua ni baba yake, akamfuata na kumuomba ampe mashamba, sikiliza maneno haya.

"Ikawa hapo alipokwenda kukaa naye, huyo mwanamke akamtaka ili aombe shamba kwa baba yake; na huyo mwanamke akashuka katika punda wake; Kalebu akamwuliza, una haja gani utakayo? Mwanamke akasema, nipe baraka: kwa kuwa wewe umeniweka katika nchi ya Negebu, basi unipe na vijito vya maji pia. Kalebu akampa vile vijito vya maji vya juu na vijito vya chini."
(WAAMUZI 1:14-15).

Aksa alifahamu kuwa baba yake ndiye aliye mpeleka huko, na ndiye mwenye wajibu wa kumtunza kwa sababu ndiye aliye mpeleka huko. Hata wewe ndugu yangu ikiwa Mungu ndiye aliye kuongoza uishi hapo. Fahamu una ujasiri wa kumwambia akupe kila unalolihitaji, neno la Mungu linasema kuwa tunatakiwa twende tukaseme naye na tukahojiane naye, ili atupe haki yetu. Ona maneno haya ya Bwana yasemavyo

"Unikumbushe; na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako" (ISAYA 43: 26).

Tunazo haki zetu nyingi sana kwa Mungu, mojawapo ni kutunzwa na yeye, sasa ona anasema tuhojiane naye, fikiri unaomba akubariki hapo ulipo, na yeye akakuhoji kuwa ni nani aliyekuambia ukae hapo au akuulize swali kama hili, Nani kakuambia uishi au ujenge hapo? Utamjibu nini? Fikiri Mungu anakuuliza nani kakuleta hapa?. Utamjibu nini? Watu wengi leo ni mafundi wa kumuomba sana Mungu awasaidie awapiganie nk wakati Mungu hakuwatuma waolewe na hao wanaume, au hata kufanya kazi wafanyazo na hili la kuishi watakapo halafu wakikwama wanakimbilia kumlazimisha Mungu awapiganie nk. Sikiliza kabla haujaenda kuomba msaada kwake, unatakiwa utubu kwanza, uombe msamaha kwa kosa lako la kutokutafuta ushauri wake, ndipo uombe msaada wa kusaidiwa naye. Na hapo unatakiwa uwe mpole kwani hatafanya kama utakavyo kwa muda utakao wewe .

Kama huna uhakika au imani kuwa Mungu anataka au amekupangia uishi hapo, iwe kwa muda au kwa maisha yako yote. Anza kufanya maombi ya ufahamu, muombe msamaha, mwambie akuongoze katika eneo alilokupangia uishi, ukikaa hapo ndipo utakua baraka, na utapata uhalali wa kutunzwa na Mungu. Hebu tusonge mbele tuone mambo mengine muhimu unayotakiwa uyafanye katika eneo hilo unalo ishi.

JIFUNZE KULIKOMBOA ENEO UNALOISHI

Sikiliza inawezekana kabisa Mungu amekupa nafasi ya wewe kuishi katika eneo fulani au eneo hilo unaloishi, iwe umepanga, au umejenga nyumba yako au umeirithi toka kwa baba yako au umelinunua. Lakini huoni mafanikio tokea ulipoanza kuishi mahali hapo mpaka unatamani kuhama, lakini Roho Mtakatifu anakuambia ukae hapo, yaani hapo ndipo Mungu anataka uishi ila huoni mafanikio kabisa, yawe ya kiuchumi au kiafya ama kifamilia hakuna amani, pia hata kiroho hauendelei upo palepale kihuduma ndio kabisa hausongi mbele. Unajiuliza ufanye nini sasa? Unajua ni kwanini hufanikiwi kwenye eneo alilokuweka Mungu uishi? Ni kwa sababu hizi zifuatazo.

1. HUJALIKOMBOA ENEO HILO KWA DAMU YA AGANO JIPYA YA YESU KRISTO.

Neno la Mungu linapozungumzia suala la nchi au ardhi hii tunayoikanyaga linaizungumzia kiajabu sana. Fahamu kuwa nchi au ardhi inaweza kubeba laana fulani kutokana na maovu wayafanyayo wanadamu.Hilo ni jambo ambalo unatakiwa ulifahamu kabla haujakwenda kuishi sehemu yoyote ile. Lazima ufahamu kuwa watu waliokuwepo hapo inawezekana walimfanyia Bwana maovu na walipoyafanya hayo maovu ardhi ilinajisika na baada ya kunajisika tu ikabeba laana, sasa haijalishi ni nani anaishi hapo, iwe ni wewe mgeni au huyo mwenyeji wote mtajikuta mnakwama kwenye masuala ya mafanikio yawe ya kiroho au kiuchumi nk.

Ona mfano huu, Adamu na mkewe walipofanya dhambi neno la Mungu linasema tendo hilo lilipofanyika tu, nchi ikanajisika na kubeba laana, au niseme nchi ikakorofishana na Adamu, ikagoma kutoa mafanikio kwa Adamu kwa kiwango atakacho Adamu. Sikiliza maneno haya ya Bwana aliyomwambia Adamu baada ya kufanya dhambi.

"Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema, usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;..."
(MWANZO 3:17)

Angalia tendo la Adamu kufanya uovu lilimgharimu kweli, kwanza hukumu ya kifo ikamkabili, pili ardhi au nchi ikabeba laana, akajikuta hana mafanikio tena kwenye eneo lile alilowekwa aishi. Kumbuka Mungu ndiye aliye mweka aishi kwenye hiyo ardhi.

Pia hata wewe inawezekana kabisa Mungu akakuweka kwenye hiyo ardhi uishi, lakini huoni mafanikio kabisa, unajua ni kwa nini huoni mafanikio? Inawezekana ni kwa sababu ardhi imenajisika na imebeba laana kwa sababu ya dhambi iliyotangulia kufanywa na hao waliotangulia kuishi mahali hapo, iwe ni kwenye nyumba hiyo unayoishi ya kupanga au hapo ulipojenga, ama watu wa eneo hilo au mji huo unaoishi. Lazima ujifunze kutubia maovu yote yaliyofanywa katika eneo hilo unaloishi, fanya maombi ya kuikomboa hiyo ardhi kwa damu ya Yesu Kristo. Unaweza kusema hivi mtumishi nifanye toba kwa ajili ya ardhi au nchi kwani hiyo nchi inasikia, inatenda au ina uhai? Sikiliza neno la Mungu linasema ardhi au sisi tumezoea kuiita nchi, inayo uwezo wa kusema na kumkataa mtu asiishi juu yake! Pia nchi inaweza kusikia , kufurahi, hata kushangilia, ina mdomo nk, ona maneno haya yanavyoizungumzia nchi.

"Ee nchi, usiogope; furahi na kushangilia; kwa kuwa Bwana ametenda mambo makuu. Msiogope, enyi wanyama wa kondeni; maana malisho ya jangwani yanatoa miche, na huo mti unazaa matunda yake, mtini na mzabibu inatoa nguvu zake. Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie Bwana, Mungu wenu....."
(YOELI 2:21-23).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Mungu anazungumza na makundi matatu. Kundi la kwanza, ni Nchi, kundi la pili ni Wanyama, na kundi la tatu ni Watu, kawaida wana wa Sayuni. Ona hapo utagundua Mungu anajua kuwa nchi, inaweza kufurahi, kushangilia na hata kuogopa, anasema nchi, shangilia, usiogope na ufurahi. Angalia mpendwa, kumbe nchi, inaweza kuogopa, kufurahi, hata kushangilia, ngoja nikuchekeshe kidogo, nchi inaweza kufurahi hata ikacheza! ikicheza ninyi mnaita tetemeko la ardhi, ebu fikiri imefurahi halafu ikacheza! Kutatokea nini kama si nchi kutetemeka?. Sikia nchi ina mdomo.

"..Nchi ikamsaidia mwanamke; nchi ikafunua kinywa chake, ikaumeza mto ule aloutoa yule joka kinywani mwake.".
(UFU 12:16-).

Umeyasikia maneno hayo yasemavyo, anza kuiangalia nchi kama Mungu anavyoiangalia, neno linasema nchi, ilimsaidia huyo mwanamke, fikiria kwa upana kuwa nchi inaweza kutumika kumsaidia mtu au kumwangamiza! Ina mdomo, kama iliweza kuyaona hayo maji basi pia ina macho yake! Pia inaweza kusikia, kama Mungu anaiambia sikia ee nchi! basi nchi ina masikio pia. Nchi inaweza kutapika maandiko yanatufundisha hivyo. Angalia maneno ya Bwana yanavyosema.

"...Msiitie unajisi katika mambo hayo hata mojawapo; kwa maana hizo taifa nitakazozitoa mbele zenu zimekuwa najisi kwa mambo hayo yote; na hiyo nchi imekuwa najisi; kwa ajili ya hayo naipatiliza uovu wake juu yake, na hiyo nchi yatapika wenyeji wake na kuwatoa kwa hiyo mtazishika amri zangu na hukumu zangu, wala msifanye machukizo hayo mojawapo; yeye aliye mzalia, wala mgeni aketiye kati yenu;(kwa kuwa hao watu wa nchi wameyafanya machukizo haya yote, hao waliotangulia mbele zenu, na hiyo nchi imekuwa najisi;) ili kwamba hiyo nchi isiwatapike na ninyi pia, hapo mtakapoitia unajisi, kama ilivyoitapika hiyo taifa iliyotangulia mbele yenu."
(LAW 18:24-28).

Ukiyasoma maneno hayo, utaona wazi kuwa, nchi inaweza kutapika. Pia Nchi huzungumza na mbingu na Mungu . ona maneno haya yasemavyo.

"Tena itakuwa siku hiyo, mimi nitaitika, asema Bwana; nitaziitikia mbingu, nazo zitaiitikia nchi;"
(HOSEA 2:21)

Mungu anasema ataziitikia Mbingu na mbingu kuitikia nchi, ona maneno hayo yanatupa ufahamu kuwa nchi inaweza kuita, au kusema hata mbingu pia.

Nimetaka uyaone maneno hayo, ili uanze kuiangalia nchi au eneo kwa picha kama hiyo, yaani unapoambiwa kuhusu kulikomboa eneo hilo nataka uwe na mwanga kuwa eneo au nchi ni kiumbe kilicho hai kabisa. Kinahitaji kuhubiriwa kabisa. Unaweza sema una maana gani Steven? Sikia neno la Mungu linasema kuwa kuna injili ya viumbe vyote ambayo tunapaswa kuifahamu na kuihubiri. Sikia Yesu asemavyo,

"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."
(MARKO 16:15).

Ona Injili iliyotajwa hapo ni Injili inayotakiwa waubiriwe viumbe vyote. Ona maneno haya.

"Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili; si kwa hiari yake, ila kwa sababu yake yeye aliyevitiisha katika tumaini; kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa."
(RUM 8:18-22).

Neno la Bwana linatufundisha kuwa, viumbe vyote vinahitaji kuwekwa huru, au kuokolewa ama kukombolewa, vinaugua, vinauchungu, kisa ni kwa sababu ya dhambi azifanyazo mwanadamu, kama dhambi ikifanywa, ardhi ndiyo inayobeba unajisi, na laana inaikalia. Fahamu ardhi hiyo inahitaji kupigwa injili ili ikombolewe, neno injili maana yake ni habari njema. **LAZIMA TUJUE KWA UNDANI HABARI HIZI ZA KUIPELEKEA HABARI NJEMA ARDHI AU KILA KIUMBE.** Sikiliza Bwana Yesu hakuja kukuokoa wewe tu, alikuja pia kuokoa kila kiumbe. Neno linasema kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, neno ulimwengu ni neno pana sana, limebeba kila kitu alichokiumba Mungu, sasa Yesu alitumwa ili aje auokoe ulimwengu pata akili hiyo. Naona sasa umeelewa kuhusu jambo la kulikomboa eneo unalo ishi. Hebu yaangaliye tena maneno haya

"Tena itakuwa siku hiyo, mimi nitaitika,asema Bwana; nitaziitikia mbingu, nazo zitaiitikia nchi; nayo nchi itaiitikia nafaka na divai na mafuta; nayo yataiitikia Yezreeli."
(HOSEA 2:21-22).

Ukiyasoma maneno hayo, utagundua kuwa nchi ina uhai, inasema, inaweza kuwasiliana na Mungu, na Mbingu pia. Kama inaweza kuwasiliana na Mungu na mbingu, basi inaweza kukusikia wewe ukiiambia neno! Na ikakuitikia kabisa. Bahati mbaya watoto wa Mungu wengi hawalijui jambo hili, huwa hawapatani na nchi, au ardhi kwa kupitia maombi. Sikiliza nchi inaweza kukukubalia wewe uishi hapo au inaweza kukukataa wewe usiishi juu yake. Angalia tena maneno haya.

"Msijitie unajisi katika mambo hayo hata mojawapo; kwa maana hizo taifa nitakazozitoa mbele zenu zimekuwa najisi kwa mambo hayo yote; na hiyo nchi imekuwa najisi; kwa ajili ya hayo naipatiliza uovu wake juu yake, na hiyo yatapika wenyeji wake na kuwatoa.....(kwa kuwa hao watu wa nchi wamefanya machukizo haya yote, hao waliotangulia mbele zenu, na hiyo nchi imekuwa najisi;) ili kwamba hiyo nchi isiwatapike ninyi pia, hapo mtakapoitia unajisi, kama ilivyowatapika hiyo taifa iliyowatangulia mbele zenu."
(LAW 18:24-28).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa, nchi ndiyo inayopeleka mapendekezo kwa Mungu kuwa fulani hafai kuishi juu yangu kwa sababu ananiumiza kwa makosa yake,

kwanini nasema hivyo? Sikiliza mwanadamu afanyapo dhambi, nchi ndiyo inayoumia, kwani inabebeshwa zigo la huo uovu, Mungu anasema inanajisika, na ikinajisika inabatiliziwa uovu huo, yaani inaambatanishiwa uovu huo. Sasa ikichoka inaamua kumtapika huyo mtu aliye juu yake! Umeelewa hapo? Kuanzia leo anza kuitazama nchi kama Mungu anavyoitazama, ukianza kuitazama kama Mungu anavyoitazama, utajifunza kufanya maombi ya toba kwa ajili ya uovu ulio juu ya nchi hiyo unayoiketi. Fahamu ukienda kuishi eneo lolote lile wewe umelinunua ni shamba, unataka kujenga, au umejenga nyumba hapo, au umepanga wenyeji waliotangulia hapo kuna maovu waliyafanya, sasa ukienda kukaa wewe utayakuta hayo maovu tu, kwani tayari yaliambatanishwa kwenye ardhi hiyo. Mwenye kuyaondoa hayo maovu ni wewe, na utayaondoa kwa kutumia damu ya Bwana Yesu Kristo. Sikiliza, jifunze kufanya maombi maalum ya kutubia maovu hayo, hata kama huyajui, omba, tumia damu ya Yesu kuondoa hayo maovu, itakase hiyo nchi, isafishe kwelikweli kama unavyojisafisha wewe mwenyewe moyoni mwako kwa kutumia damu ya Yesu Kristo. Naamini wewe unapoenda kuoga unaoga vizuri, unauondoa uchafu mwilini mwako kwa bidii sana, basi fanya hivyohivyo kuondoa uchafu ulio katika nchi, hapo ndipo nchi itakapo achilia mafanikio yako. Yawe ya kiroho au kiuchumi ama kifya na kiutumishi. Kinyume cha hapo utapelekwa na Mungu kwenye hiyo nchi, au eneo hilo unaloishi hutaona mafanikio.

Anza kuangalia je! Kwenye hilo eneo hao wenyeji wanamuabudu nani? Au huyo aliyekupangishia hiyo nyumba anamuabudu nani? fuatilia hapo ulipopanunua huyo aliyekuuzia aliweka nini kwenye ardhi, kama hamuabudu Mungu, nakuambia ni rahisi sana kwa watu wanamna hiyo kuweka miungu kwenye ardhi. Inawezekana kuna matambiko yaliwekwa kwenye hiyo ardhi, wewe unaenda kukaa hapo mahali ambapo tayari ardhi imenajisika, na imebeba mapepo nk. Fikiri umenunua ardhi sehemu ambayo damu ya mtu ilimwagwa, nakuambia ukweli, sehemu hiyo kukupa mafanikio inakua ngumu sana hata kama Mungu yupo. Sikiliza maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Hivi hamtaitia unajisi nchi ambayo mwakaa; kwa kuwa damu huitia nchi unajisi; wala hapana sadaka itoshayo kwa ajili ya nchi, kwa ajili ya damu iliyomwagwa ndani yake, isipokuwa ni damu ya huyo aliyeimwaga. Kwa hiyo msiitie unajisi nchi muiketiyo ambayo naketi nami kati yake; kwa kuwa mimi Bwana naketi kati ya wana wa Israeli."
(HESABU 35:33-34)

Ukiyaangalia maneno hayo utagundua ni kwa nini watoto wa Mungu wengi hawafanikiwi kwa sababu ya kizuizi hiki cha eneo wanaloishi tena wanaishi pamoja na Mungu. Sikiliza Mungu anaketi na sisi pale anapotuambia tuishi sehemu fulani, sasa ikiwa sehemu hiyo damu ya mtu au watu ikimwagwa, neno linasema nchi au ardhi inanajisika, ardhi ambayo unakaa ikoje! Kweli unaye Mungu hapo, mnaishi wote, lakini ardhi hiyo, imenajisika kwa sababu ya damu nyingi za watu zilizomwagwa, iwe ni katika magomvi, ajali, polisi kuuwa watu, iwe kwa ujambazi au kwa kujiua nk. Ona jinsi wanawake wengi watoavyo mimba na damu inamwagika na kuitia nchi unajisi, na bahati mbaya Wakristo wengi

hawajui madhara ya hiyo damu iliyomwagika kwenye ardhi yao. Fikiri leo walemavu wa ngozi, wanauwawa damu inamwagika, au watoto kubakwa na kuuwawa kwa imani za kishirikina. Wakristo wengi hawayaoni madhara yake, wanafikiri kwa kuwa si wao waliofanya hivyo basi watabarikiwa tu, sikiliza mpendwa. Ikimwagwa damu ardhi inanajisika, na ikinajisika inaiambia mbingu kuwa isinyeshee mvua, haijalishi wanaoishi hapo ni wana wa Mungu au la. Mvua isiponyesha wote wataumia waliomwaga damu na hao wasio mwaga hiyo damu. Mpaka toba ifanyike. Ona mfano huu mzuri.

"Kulikuwa na njaa siku za Daudi muda wa miaka mitatu, mwaka kwa mwaka; naye Daudi akautafuta uso wa Bwana, Bwana akasema, ni kwa ajili ya Sauli. Na kwa nyumba yake yenye damu, kwa kuwa aliwaua hao Wagibeoni."
(2SAMWELI 21:1)

Neno la Mungu linasema, nchi ya Israeli ilijikuta kwenye tatizo la njaa kali kwa muda wa miaka mitatu na nusu, kisa ilikuwa ni dhambi ya umwagaji wa damu alioufanya mfalme Sauli wakati wa utawala wake. Sikiliza Sauli aliwauwa hao Wagibeoni, baadaye akafa, akaanza kutawala Mfalme Daudi, miaka ikapita, siku moja ghafla, mbingu ikagoma kuachilia mvua. Fikiri damu aliimwaga Sauli si Daudi, lakini cha moto anakipata Daudi kwa nini? Tena siku mvua inagoma kunyesha haikuwagomea wenye dhambi tu, iliwagomea watu wote wanaoishi kwenye hiyo aridhi. Haikuangalia huyu ni Kuhani au huyu ni Nabii, haikumwangalia Mfalme Daudi mteule aliyepakwa mafuta mara tatu, iliwakatalia wote. Kwa lugha nzuri niseme madhara ya damu ya hao Wagibeoni yaliwakumba watu wote, walioimwaga na hao wasioimwaga. Kumbuka damu ilipomwagika nchi ikanajisika, ilipochoka, ikafanya mawasiliano na mbingu, ikamwambia mbingu, usiachiliye mvua. Kisa, kuna damu imemwagwa. Mpaka toba ilipofanyika ndipo mvua ilinyesha. Umeona hapo? Sasa wewe unakaa kwenye eneo la namna gani? Unajua kizuzi cha mafanikio yako kinatokana na eneo hilo unaloishi? Anza leo kulikomboa kwa kutumia damu ya Yesu Kristo. Ukianza kufanya maombi ya namna hiyo, nakuambia ukweli utaanza kuona mafanikio katika maisha yako, yawe ya kiroho au kiuchumi,au kihuduma.

Jambo linalopelekea leo hii kudhoofisha uchumi wa watu wengi ni dhambi, ziwe zile zilizofanyika huko nyuma na waliotangulia, au zinazofanywa sasa na watu. Ukiyasoma maneno haya ya Mungu, yanafichua sababu inayopelekea watu kudhoofu au kutofanikiwa kwenye kila kona. Sikiliza asemavyo Bwana.

"Lisikieni neno la Bwana, enyi wana wa Israeli; kwa maana Bwana ana mateto nao wakaao katika nchi, kwa sababu hapana kweli, wala fadhili, wala kumjua Mungu katika nchi. Hapana neno ila kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu. KWA AJILI YA HAYO NCHI ITAOMBOLEZA, NA KILA MTU AKAAYE NDANI YAKE ATADHOOFIKA, pamoja na wanyama wa kondeni na ndege wa angani; naam, samaki wa baharini pia wataondolewa"
(HOSEA 4:1-3).

Nchi, huwa inaomboleza yaani inalia kwa sababu ya hayo maovu. Leo angalia katika nchi yetu hii, utaona maovu hayo ndiyo yanayotendeka sana, unafikiri utapona kudhoofika? Angalia damu zinavyomwagwa, ona uzinzi unavyofanyika, vyote hivyo vikifanyika ardhi inanajisika na inabeba laana (kudhoofisha) ndio maana huoni mafanikio. Mpaka utakapojifunza kutubia maovu hayo na kumuomba Mungu aitakase hiyo nchi au ardhi unayoishi.

Mungu anakusubiri wewe, ardhi pia inakusubiri wewe uanze kusema kuhusu utakaso wa hiyo ardhi, usipomwambia Mungu asamehe, na atakase hiyo ardhi, fahamu hataitakasa, mpaka wewe utakapo anza kumwita na kumwambia aje, na atakase, na kuondoa kila laana kwenye hiyo ardhi. Yesu Kristo anatufundisha anasema lazima tujifunze kusali, na tumwambie Mungu Ufalme wake uje hapa duniani. Sikia kama tusipomwomba aulete huo Ufalme wake fahamu hatauleta. Kama tunataka leo aje kwenye maeneo tunayo ishi lazima tujifunze kuyatakasa hayo maeneo kwa maombi kwa kutumia damu ya Yesu Kristo iitwayo **DAMU YA AGANO JIPYA YA BWANA YESU KRISTO**. Sikiliza neno la Mungu linasema kila kitu kinatakiwa kitakaswe kwa kutumia damu. Ona

"Na kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya, ili mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele. Maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya. Kwa hiyo hata lile la kwanza halikuanzwa pasipo damu. Maana kila amri ilipokwisha kunenwa na Musa kwa hao watu wote, kama ilivyoamuru sheria, aliitwaa damu ya agano mliloamriwa na Mungu. Na ile hema nayo na vyombo vyote vya ibada alivinyunyuzia damu vivyo hivyo. Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu. Na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo"
(EBR 9:15-22)

Hebu rudiarudia kuyasoma maneno hayo utagundua vitu vingi sana vilivyopo hapo ndani. Neno la Mungu linasema Yesu Kristo ndiye mjumbe wa agano jipya. Fahamu maagano yote yalikuwa yanafungwa kwa kutumia damu. Yesu kama mjumbe wa agano jipya anayo Damu aliyoimwaga yeye mwenyewe, Damu hiyo ndiyo, inayoyaondoa maagano yote yaliyomtangulia, sikiliza neno la Mungu linasema kila kitu kilisafishwa kwa kutumia damu, hata leo ndio hivyo hivyo. Bahati mbaya Wakristo wengi wanajua kujisafishia dhambi tu. Sikiliza, Damu hiyo ya Yesu, ndiyo inayoweza kulipa fidia ya damu zote zilizomwagwa. Ziwe zilizomwagwa na watoa mimba, polisi, watu waliowauwa na watu kwa kuitwa wezi, au watu waliouwawa na majambazi, ajali, vita, hata na washirikina. Sikiliza, ukisimama leo hii kwa imani, na ukaomba msamaha, kwa ajili ya hizo damu, na ukaitumia Damu ya agano jipya ya Bwana Yesu Kristo kuondoa maagano yote yaliyofungwa kwenye ardhi, nakuambia ukweli maagano ya kale yatateketezwa na Damu ya Agano jipya ya Bwan Yesu Kristo. Sikiliza leo hii kuna watu wamefunga maagano na nguvu za giza kwa kupitia damu za watoto wao, au kwa kutumia damu

za watu wengine nk ili wapate vyeo au mali. Sikiliza ukisimama wewe na kuamua kuyavunja hayo maagano kwa kutumia Damu ya Agano jipya ya Bwana Yesu Kristo nakuambia ukweli maagano ya kale lazima yaondolewe!

Anza leo hii kuitia hiyo Damu ya Agano jipya ya Bwana Yesu Kristo. Kwenye eneo unaloishi, tubia maovu yote yaliyo katika hilo eneo, yaliyokaa kwenye ardhi, ondoa huo unajisi ulio katika hiyo ardhi. Tumia Damu hiyo kuyaondoa hayo **OMBA MUNGU KILA SIKU AACHILIE DAMU YAKE HIYO KWENYE HIYO ARDHI AU MAHALI POPOTE PALE UTAKAPOKUWEPO.** Hapo ndipo tutakapoanza kuona mafanikio katika mambo yetu yote. Sikiliza maneno haya

"Na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa inenayo mema kuliko ile ya Habili"
(EBR 12:24).

Damu ya Yesu pekee ndiyo inayoweza kuzima mashitaka ya damu ishitakio kutoka katika ardhi, kumbuka damu ya Habili ndiyo ilipeleka mashitaka kwa Mungu ikitokea ardhini. Sasa jifunze kuiita Damu ya Yesu ili inene mema kutoka katika hiyo ardhi uliyopewa uishi na Bwana Mungu. Ni imani yangu kuwa umenielewa vizuri, na umegundua ni kwanini umekwama hapo ulipo. Mungu yupo tayari leo kukukwamua kwa kukuondolea hicho kizuizi kilichotokana na unajisi ulipelekea laana kwenye nchi au ardhi unayoishi, tendea kazi hayo uliyojifunza utafanikiwa.
Hebu tusonge mbele tuone maombi mengine ambayo unatakiwa uyaombe kila siku kwa ajili ya eneo unaloishi.

JIFUNZE KILA MARA KULIOMBEA AMANI ENEO UNALOISHI

Moja ya jambo kubwa ambalo unatakiwa ulifanye katika kuliombea hilo eneo unaloishi ni hili la kuliombea amani eneo hilo unaloishi. Mungu aliwapeleka wana wa Israeli huko Babeli, na aliwafundisha jambo la kufanya nalo lilikuwa ni la kuutakia mji huo amani.

"Kautakieni amani mji ule, ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa Bwana; kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani."
(YEREMIA 29:7).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua wazi kuwa, Mungu aliwaagiza hao wana wa Israeli wamuombee ili aweke amani katika mji watakaoingia kuishi hao wana wa Israeli. Hebu fikiri, kwanini Mungu awaambie hao wana wa Israeli kuwa wamuombe aweke amani katika mji huo badala ya yeye kuweka amani katika mji huo bila kumwomba? Unajua watoto wa Mungu wengi sana wanafikiri Mungu ataweka amani katika miji wanayoishi bila wao kumuomba Mungu aweke amani katika miji hiyo. Sikia usipomuomba Mungu aachiliye amani katika mji unaoishi, hata weka amani katika mji huo. Kama mji utakuwa

na amani, ndipo hata wewe utakuwa na amani, ndivyo Mungu alivyosema. **"kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani"** Kama mji huo hauna amani, basi hata wewe mtoto wa Mungu hutakuwa na amani kabisa! Sikia mji ukikosa amani, unapelekea dhambi, unapelekea magonjwa, wezi, ukahaba, kutofanikiwa nk.

Magonjwa yanapoupiga mji, yanaondoa amani kabisa, na yapo magonjwa ambayo huyakuti katika miji mingine, ila kwenye mji fulani tu. Fikiria kwenye mtaa wenu kukoje, kuna amani kweli? Mbona huko ndiko kuna vibaka, wezi, wachawi wanaologa mafanikio ya watu na ya kwako pia! Lazima ubadilishe mfumo wa maombi yako, uanze kumuomba Mungu aweke amani katika mji huo unaoishi, amani ikikosekana katika mji huo fahamu hutafanikiwa kabisa, sikia leo kukitokea vita kwenye mji unaoishi, huwezi kufanya biashara, kulima, au hata kufanya kazi, wewe fuatilia miji ambayo vita inapiganwa huko utagundua ninalokuambia. Moja ya kosa kubwa tunalolifanya watoto wa Mungu ni hili la kutokuwa na maombi kwa Bwana ili aachiliye amani yake katika miji tunayoishi. Anza leo hii kuomba maombi ya namna hii kila siku.

JIFUNZE KUUNENEA MEMA MJI HUO UNAOISHI

Kama leo unataka kuubadilisha mji huo utoke katika hali ya laana iliyoukalia mji huo unaoishi lazima ujifunze kuanza kuunenea mema mji huo. Usikubaliane na maneno yoyote yale mabaya ambayo mji wako unanenewa. Unene mema mji wako unaoishi, usemee maneno mema. Kwa mfano kama kwenye mji wenu hakuna mafanikio ni mji ambao watu wanasema mji huo hauna mzunguko mzuri wa fedha. Badilisha hayo maneno kwa kuyakataa hayo maneno anza kuunenea mema. Sikia neno la Mungu linasema Mungu anaumba matunda ya vinywa vyetu**.**

"Mimi nayaumba matunda ya midomo;.."
(ISAYA 57:19)

Mungu anaumba matunda ya midomo yetu, anza kuumba pamoja na Mungu, kwa kuunenea mji huo maneno mema ndipo Mungu atayaumba mema kwenye huo mji. Ukiangalia kwenye kitabu cha **Mithali** maneno ya Bwana yanasema hivi.

"Tumbo la Mtu litajazwa matunda ya kinywa chake; atashiba mazao ya midomo yake. Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na wao waupendao watakula matunda yake."
(MITHALI 18 :20-21).

Mungu anakusubiri wewe uanze kuunenea mema mji huo unaoishi ili mji huo uanze kuachilia baraka ambazo zitakuwasilia wewe na jamii yote inayokuzunguka.

TAKASA JINA LA MJI HUO

Moja ya jambo unalotakiwa ulifanye katika maombi yako kila mara, jifunze kulitakasa jina la mji huo unaoishi. Sikia mji unaweza kubeba upako unaotokana na jina lake. Kama mji una jina baya, fahamu jina hilo litapitisha mabaya katika mji huo. Kuna majina mengi sana ambayo miji imepewa, ukiyaangalia kiroho, utagundua ninachokuambia, majina hayo yamebeba mabaya ambayo yameathiri tabia ya watu wanoishi kwenye miji hiyo. Wewe fanya utafiti huu utaona ninachokuambia, anza kufanya utafiti wa jina la mji wenu maana yake nini. Na ni nani aliyetoa jina hilo. Majina mengi tunatoa kutokana na sifa za mji, mtu fulani, nk sasa sikia kama mji una jina la mtu maarufu, je! Nini maana ya jina lake? na huyo mtu alikuwa na sifa gani? Unajua kuna mambo watu wanayafanya ila hawajui madhara yake, watu wapo tayari kutoa majina kwa watoto wao au miji bila kufahamu madhara na mazuri yanayoweza kupita kwa kupitia jina hilo.

Sikia, Mungu alilazimika kuwabadilisha watu wengi tu majina yao kwa sababu aliona madhara yaliyomo ndani ya majina ya watu hao, hata majina ya miji, ukisoma maandiko matakatifu utagundua miji mingine ilibadilishwa majina yao. Kwa nini yalibadilishwa? Ni kwa sababu yalibeba mabaya, ambayo Mungu aligundua kuwa yatapitisha mabaya. Ngoja nikupe mifano hii.

"Akasema, niache, niende, maana kunapambazuka akasema, sikuachi, usiponibariki. Akamwuliza, jina lako n'nani? Akasema, Yakobo. Akamwambia, jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu nawe umeshinda." (MWANZO 32:26-27).

Ukiangalia maneno hayo utaona wazi kuwa Mungu aliamua kumbadilisha jina Yakobo akampa jina la Israeli. Hata Ibrahimu alimbadilisha jina, aliitwa kwanza Abramu akampa jina la Ibrahimu, hata Sara, pia aliitwa Sarah akamwita Sara. Hata Luzu ulibadilishwa ukaitwa Betheli

"Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe alililoliweka chini ya kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake. Akaita jina la mahali pale Betheli; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu" (MWANZO 28:13-19).

Mji wenu unaitwa jina gani? Hebu anza kulitakasa jina la mji wenu kwa damu ya Yesu Kristo.

OMBEA ULINZI KATIKA MJI WENU

Ukisoma maandiko matakatifu utagundua kuwa, Mungu ameweka walinzi katika kila mji. Sikia wapo walinzi wa mji. Ona maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kumi na moja, yaani mwezi uitwao Shebati, katika mwaka wa pili wa Dario, neno la Bwana lilimjia Zekaria, mwana wa Berekia, mwana wa Ido, nabii, kusema, naliona wakati wa usiku, na tazama, mtu amepanda farasi mwekundu, akasimama kati ya mihadasi iliyokuwa mahali penye utulivu; na nyuma yake walikuwapo farasi wengine wekundu, na rangi ya kijivujivu, na weupe. Ndipo nikasema. Ee Bwana wangu, ni nini hawa? Basi yule malaika aliyesema nami akaniambia, nitakuonyesha ni nini hawa. Na yule mtu aliyesimama kati ya mihadasi akajibu, akasema, hawa ndio Bwana aliowatuma, waende huko na huko duniani. Nao wakamjibu yule malaika wa Bwana aliyesimama kati ya mihadasi, wakasema, Tumekwenda huko na huko duniani, na tazama, dunia yote inatulia, nayo imestarehe."
(ZEKARIA 1:7-11).

Ukiyaangalia hayo maneno ya Bwana, utagundua kuwa, kuna viumbe wanaofanya kazi ya kuzunguka duniani kote, ili wapate kuona ni kitu gani kinachoendelea, neno linasema wametumwa na Bwana. Wakizunguka ndipo wanapoleta jibu kwa huyo malaika, na huyo malaika ndipo anapopeleka taarifa kwa Mungu. Soma maneno haya utaona hicho ninachokuambia**.**

"Ndipo yule malaika wa Bwana akajibu, akasema, Ee Bwana wa majeshi, hata lini utakataa kuurehemu Yerusalemu, na miji yote ya Yuda ulioikasirikia miaka hii sabini?
(ZEKARIA 1:12).

Katika ulimwengu wa roho hayo mambo yanatendeka kabisa. Ukianza kuombea mji huo ulinzi kutoka kwa Mungu, ndipo hao wazungukao na kuona kila kinacho endelea watapeleka taarifa kuwa sehemu fulani, watu wa eneo hilo wanahitaji ulinzi, au kuokolewa katika uonezi wa nguvu za giza. Ukikaa kimya nao watakaa kimya. Ona mfano huu mwingine wa walinzi wa mji.

"Kisha akalia kwa sauti kuu masikioni mwangu, akisema, Waamuru wale wanaousimamia mji wakaribie, kila mmoja na awe na kitu chake cha kuangamizia mkononi mwake. Na tazama, watu sita wakaja, wakitokea kwa njia ya lango la juu, lielekealo upande wa kaskazini, kila mmoja ana kitu chake cha kufisha mkononi mwake; mtu mmoja kati yao amevaa bafta, naye anakidau cha wino cha mwandishi kiunoni, wakaingia, wakasimama karibu na madhabahu ya shaba. Na huo utukufu wa Bwana wa Israeli ulikuwa umepanda juu kutoka kwa kerubi, ambaye ulikuwa juu yake mpaka kizingiti cha nyumba; akamwita mtu yule aliyekuwa amevaa bafta mwenye kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. Bwana akamwambia, pita kati ya mji, kati ya Yerusalamu, ukatie alama katika vipaji vya nyuso vya watu wanaougua na kulia kwa sababu ya

machukizo yote yanayofanyika kati yake. Na hao wengine aliwaambia, nami nalisikia , piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachie, wala msione huruma; waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni patakatifu pangu, basi wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba."
(EZEKIELI 9:1-6).

Hayo mambo Ezekieli alionyeshwa yakitendeka kwenye ulimwengu wa roho, na yakadhihirishwa kwenye ulimwengu huu unaoonekana kwa macho haya ya nyama. Hao wasimamizi wa mji wanaotajwa hapo, ni viumbe vilivyoko katika ulimwengu wa roho, aliwaona makerubi. Pia aliwaona viumbe wengine yeye amewaita watu. Neno mtu ni mfano wa Mungu yaani roho, Mungu anaposema na tufanye mtu kwa mfano wetu anazungumzia roho. Nataka uone ninachokiona kwenye maneno hao, kuna viumbe au wasimamizi wa miji, ambao kazi yao ni kuusimamia mji, wanapokea amri ya kufanya jambo kutoka kwa Bwana. Tena huyo mwingine kazi yake yeye ni kuandika taarifa zote za mji huo. Umeelewa hapo? Mtu huyo ndiye aliyepewa agizo la kuweka alama kwenye paji za nyuso za watu waliokuwa wanaulilia mji au wanaouombea mji huo. Watu waliokuwa wakifanya kazi ya kuuombea mji huo ndio waliopona. Hebu fikiri, wewe unaishi kwenye mji gani? Unajua kuwa katika mji huo kuna viumbe hao? Sikia wapo. Wanakusubiri wewe uanze kuuombea mji huo ulinzi, ndipo utashangaa mji wenu huo unaanza kupokea ulinzi madhubuti kutoka kwa Mungu, Mungu atawapigania na kuondoa, ajali, magonjwa, mapepo nk katika mji wenu huo mnaoishi.

ANZA KUTUBIA MAOVU YA HUO MJI UNAOISHI

Sikia ndugu. Kuna miji ambayo Mungu ameikasirikia kabisa kwa sababu ya maovu yaliyomo kwenye miji hiyo. Ona mfano huu.

"Ndipo yule malaika wa Bwana akajibu, akasema, Ee Bwana wa majeshi, hata lini utakataa kuurehemu Yerusalamu, na miji yote ya Yuda ulioikasirikia miaka hii sabini?
(ZEKARIA 1:12)

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi kuwa, Mungu aliikasirikia miji hiyo, sasa kama Mungu ameikasirikia miji, sisemi watu nasema miji. Ikiwa wewe ndugu leo hii unaishi kwenye mji ambao Mungu ameukasirikia na amini upo kwenye hatari sana ya kungamizwa na Bwana. Au na adui shetani. Mungu akiuukasirikia mji, anaondoa ulinzi wake hapo ndipo mabaya yanapouvamia mji huo,anza leo hii kuuombea msamaha mji huo unaoishi. Ona Mungu aliukasirika mji wa Ninawi. Aliamua kuungamiza kabisa, watu wa mji huo waliamua kutubia makosa yao, ndipo mji huo uliposalimika. Soma kitabu chote cha Yona, utaona ninachokuambia

"Basi Yona akaanza kuuingia mji mwendo wa siku moja, akapaza sauti yake , akasema, baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa. Basi watu wa Ninawi wakamsadiki Mungu; wakatangaza kufunga, wakajivika nguo za magunia, tangu yeye aliye mkubwa hata mdogo."
(YONA 3:4-5).

Mungu alikasirika sana, akaamua kuuangamiza mji wa Ninawi, fahamu ungeamizwa huo mji ,hata watu wanaoishi kwenye huo mji wangeangamia. Watu wa Ninawi walifunga na kuomba msamaha kwa Mungu. Mungu aliwasamehe, akaacha mpango wake wa kuuangamiza huo mji wa Ninawi. Ndani ya maandiko matakatifu utaona miji mingi iliangamizwa kabisa kama Sodoma na Gomora, kisa Mungu aliikasirikia. Nataka nikuulize swali je! Wewe unaishi katika mji wenye sifa gani? Hazifanani na Sodoma na Gomora? Usikae kimya na kujifariji kuwa wewe hutendi dhambi. Mungu anataka uanze leo kuulilia mji wako huo kwa kutubia maovu yake yaani maovu ya mji wenu. Ili akuweke alama. Kama hauombi eti unafikiri kwa sababu umeokoka, basi Mungu atakapopitisha laana katika mji huo wewe utapona, sikia utapona iwapo tu, unakesha na kuuombea mji huo. Kama hauombi, hata kuwekea alama, ona maneno haya tena.

"Bwana akamwambia, pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, ukatie alama katika vipaji vya nyuso vya watu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake. Na hao wengine aliwaambia, nami nalisikia , piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachie, wala msione huruma; waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni patakatifu pangu, basi wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba."
(EZEKIELI 9:1-6).

Mungu aliagiza watu wa kwanza kuangamizwa wawe wale waliopo patakatifu pake. Yaani wanaoshinda kwenye hekalu lake. Leo hii niseme wanaoshinda kanisani. Fikiri hao wazee walikuwa ni wazee wanaoisimamia nyumba ya Bwana. Lakini walikosa alama, waliangamia. Leo hii watoto wa Mungu wengi hawana muda wa kuiombea miji yao, mabaya yanawakuta kama hawa ndugu waliokutwa na mabaya mjini Yerusalemu. Badilika ombea mji wako msamaha kwa Mungu. Ndipo utaona mafanikio katika maisha yako, mji utaanza kupitisha baraka wala si laana tena.

FANYA MAOMBI YA KUUTEKA AU KUUMILIKI MJI HUO

Ili leo hii upate kumiliki eneo ambalo Mungu amekupa ni lazima ujifunze kuliteka au kufanya maombi ya vita ya kuteka hilo eneo ambalo Mungu amekupa. Sikia ikiwa leo hii Mungu amekujulisha kuwa eneo alilokupa wewe ili uishi ni eneo fulani, au ikiwa unaishi katika mji fulani, ili mji huo wewe uumiliki inatakiwa ujifunze kufanya

maombi ya kulimiliki hilo eneo. Watoto wa Mungu wengi leo hii hawana maeneo yao wanayoyamiliki na kuyatawala. Yaani watoto wa Mungu wengi hawana mashamba yao, viwanja vya kujenga nyumba, au nyumba zao wenyewe, unajua ni kwanini?

Ni kwa sababu, adui hapendi wala hatakubali kuona watoto wa Mungu wakiimiliki nchi. Mpango wa Mungu ni kukuona wewe mtoto wake ukimiliki juu ya nchi**.**

"Nao waimba wimbo mpya wakisema, wastahili wewe kuitwaa kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi"
(UFU 12:9-10).

Mpango wa Mungu baada ya kukununua wewe na mimi ni huo wa wewe na mimi tumiliki juu ya nchi, si kumiliki tu bali na kutawala. Adui hataki kabisa kuona wewe unamiliki na unatawala juu ya nchi, yaani ukiwa unasimamia ardhi yako, shamba lako, nyumba yako, nk. Ngoja nikupe mfano huu uone, wana wa Israeli walipewa nchi ya Kanani ili waimiliki na waitawale. Mungu akawafundisha kuwa, ili waimiliki hiyo nchi ni lazima wapigane vita. Ona maneno haya yasemavyo**.**

"Tukageuka tukapita njia ya bara ya Moabu. Bwana akaniambia, usiwasumbue Wamoabi, wala usishindane nao katika mapigano; kwa kuwa sitakupa katika nchi yake kuimiliki; kwa sababu Ari nimewapa wana wa Lutu kuimiliki."
(KUM 2:8B-9).

Ukiyasoma maneno hayo ya Bwana utaona wazi kuwa katika maeneo yale ambayo Mungu aliwapa wana wa Israeli ili wapate kuyamiliki, iliwalazimu kuwasumbua hao waliokaa katika maeneo hayo na kupigana nao. Hata leo hii kama unataka kulimiliki eneo ambalo Mungu amekupa, ni lazima ujifunze kufanya maombi ya kivita, yaani maombi ya kuliteka hilo eneo. Sikia zamani walipigana kimwili, na Mungu ndiye aliye wapigania, alimtuma hata Mikaeli awapiganie. Ona maneno haya ya Bwana yasemavyo

"Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia, tazama, mtu mume akasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa na upanga wazi mkononi mwake; Yoshua akamwendea, na kumwambia, je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu! Akasema, la, lakini nimekuja sasa, nili amiri wa jeshi la Bwana. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mtumishi wake? Huyo amiri wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, vua viatu vyako miguuni mwako; kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni patakatifu. Yoshua akafanya vivyo"
(YOSHUA 5:13-15).

Amiri wa jeshi la Bwana ni Mikaeli. soma maneno haya,

"Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako;..."
(DANIELI 12:1)

Leo hii tunapigana katika ulimwengu wa roho, sikia katika ulimwengu wa roho, adui anakuzuia wewe usimiliki eneo, yaani usifanikiwe kuwa na nyumba yako, shamba lako, nk.Ili ufanikiwe lazima ujifunze kufanya maombi ya namna hiyo. Fanya maombi yafutayo. Inawezekana kabisa Mungu kakuweka au kakupa eneo hilo, lakini kuna vikwazo sana vya wewe kulimiliki eneo hilo, au inawezekana kabisa mume wako alinunua eneo hilo, lakini alipokufa ukadhulumiwa, au ni eneo la urithi wenu kabisa lakini kuna watu wanaishi hapo. Sikia usikate tamaa, jifunze kufanya maombi maalumu ya kuliteka eneo hilo na kulimiliki, tunaanza kumiliki kwanza kwenye ulimwengu wa roho ndipo tunakipata kwenye ulimwengu wa mwili. Sasa anza kufanya mambo yafuatayo.

WEKA ALAMA KATIKA ENEO HILO

Jifunze kuliwekea eneo hilo alama maalum, ona mfano huu, Mungu alipompa Ibrahimu nchi ya Kanani, alimwambia alikanyage eneo hilo**.**

"Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na magharibi; maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, na uzao wako nao utahesabika. Ondoka, utembee katika nchi hii, katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo. Basi Abramu akajongeza hema yake, akaja akakaa kwenye mialoni ya Mamre, nayo ni miti iliyoko Hebroni, akamjengea Bwana Madhabahu huko"
(MWANZO 13: 14-18).

Mungu alipompa Ibrahimu nchi hiyo, fahamu kulikuwa na watu wanaishi humo, wamejenga nyumba zao, nk. Mungu hakumwambia Ibrahimu ainunue. Alimwambia atembee na aikanyange nchi hiyo kwa mapana yake, na marefu yake! Ona jambo hilo kwa makini sana, anapomwambia alikanyange na atembee kumbuka ndipo alipokuwa anaweka alama katika ulimwengu wa roho. Na alipokuwa analikanyanga ndipo alipokuwa analimiliki, sikia kukanyaga kwa namna hiyo si kule kukanyaga kwa kawaida. Ni kufanya kitu kwa kumaanisha, yaani kumiliki eneo hilo na kulifanya lako, hata kama watu wanaishi nk. Sikia Mungu alimfundisha jambo hilo hata Yoshua, alimwambia hivi**.**

"Ikawa baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema. Musa mtumishi wangu amekufa; haya

basi, ondoka, vuka mto huu wa Jordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli, kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu nimewapa ninyi, kama nilivyomwapia Musa."
(YOSHUA 1:1-3).

Mungu alimwambia Yoshua kama vilevile alivyomwambia Ibrahimu, alimwambia kila sehemu ambayo amewapa wao wana wa Israeli waishi inatakiwa walikanyage eneo hilo, kitendo cha kulikanyaga eneo hilo alilowapa, kinawapa uhalali wa kulimiliki eneo hilo. Narudia tena jifunze kulikanyanga eneo hilo ulilopewa iwe tayari umejenga, au ni shamba, fanya jambo hilo leo, likanyage, lifunike kwa damu ya Yesu, limiliki wewe na uzao wako, unapolikanyaga eneo lako hilo, tumia jina la Yesu kumiliki eneo hilo, vunja kila roho mbaya iliyo kwenye eneo hilo. Ikiwa bado hujalimiliki, yaani inawezekana ulidhulumiwa, au ni kiwanja ambacho Bwana amekuambia ni chako, lakini huna fedha za kununua kama Ibrahimu, usiogope, kanyaga eneo hilo, linenee maneno ya kulimiliki, lifunike kwa damu ya Yesu Kristo, tulia, kuna siku utashangaa, unalimiliki, kumbuka tunamiliki kwanza kwenye ulimwengu wa roho. Usipoishi wewe hapo, wataishi wanao au wajukuu nk. Kumbuka Ibrahimu, hakuishi yeye pale walikuja kuishi watoto wake na wajukuu zake.

ANGALIZO

Usilikanyage eneo ambalo hujapewa, yaani si lako, Si kila eneo umepewa wewe, kuna maeneo wamepewa watu wengine, nataka ukanyage kwenye eneo ulilopewa wewe tu. Mungu aliwaambia wana wa Israeli, wasilikanyage kwa kulimiliki eneo walilopewa wana wa Lutu.

"Tukageuka tukapita njia ya bara ya Moabu. Bwana akaniambia, usiwasumbue Wamoabi, wala usishindane nao katika mapigano; kwa kuwa sitakupa katika nchi yake kuimiliki; kwa sababu Ari nimewapa wana wa Lutu kuimiliki."
(KUM 2:8B-9).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa si kila eneo walipewa wana wa Israeli. Hata siku ile Mungu anamwagiza Yoshua kuwaingiza wana wa Israeli alimpa mipaka, ona.

"Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu nimewapa ninyi, kama nilivyomwapia Musa. Tangu jangwa hili na Wahiti, tena mpaka bahari ile kubwa upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu. Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala kukuacha."
(YOSHUA 1:3-5).

Mungu alimpa Yoshua mipaka, na ndani ya mipaka hiyo ndimo wana wa Israeli walitakiwa watembee na kila watakapo kanyaga patakuwa pao. Naamini umenielewa.

Alama nyingine ambayo unaweza kuiweka ni kama hii. Angalia maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Na tazama, Bwana amesimama juu yake, akasema, mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii, uilalayo nitakupa wewe na uzao wako. Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kaskazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa. Tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia. Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, kweli Bwana yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. Naye akaogopa akasema, mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni. Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe alililoliweka chini ya kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake. Akaita jina la mahali pale Betheli; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu" (MWANZO 28:13-19).

Yakobo aliweka mafuta katika jiwe, ona jambo la kwanza alichukua jiwe alilokuwa amelilalia mahali pale, akalitumia kama alama, alilisimamisha, ona leo hii ukipata kiwanja halali kutoka serekalini, huwa wanakupa jiwe maalumu la kutambulisha uwanja wako. Na ndipo unapopewa na hati miliki, sasa sikia, Yakobo aliweka alama hiyo kwa imani katika eneo alilopewa na Bwana, akaamini, akaweka alama yake, kumbuka eneo hilo walikuwa wanaishi watu wengine. Jambo la pili, aliliwekea jiwe hilo mafuta. Ona hapo pana alama nyingine ya pili, aliliwekea jiwe hilo mafuta. Mafuta Kibiblia ni alama ya Roho Mtakatifu, tunaita upako. Unaweza kuchukua mafuta, ukayaombea ili Roho Mtakatifu akae ndani yake, na akuwezeshe kulipata eneo hilo. Sikia ndugu kama ulidhulumiwa nenda eneo hilo, tafuta hekima kwa Bwana, usifanye kila mtu anakuona uwe na akili, labda liwe eneo ambalo tayari ni mali yako, kama eneo hilo umepewa lakini wanamiliki hao waliokunyan'ganya kwa kukudhulumu kwa sababu ya fedha zao nk, fanya hivyo kwa hekima, weka alama, mwamini Mungu, teka eneo hilo kwa maombi ndipo utakapofanikiwa kulimiliki eneo hilo. Hebu tumalizie kwa namna hii, nasema anza kuomba sana kwa ajili ya eneo hilo unaloishi, jifunze kufanya maombi ya kuliamuru eneo hilo unaloishi lianze kupitisha mafanikio yako, yawe ya kiroho, kichumi, kiutumishi nk. Pia omba mara kwa mara kwa Mungu ili akupeleke katika eneo analotaka uishi. Fanya maombi hayo kila mara, muombe akusaidie usihamishiwe eneo lile ambalo yeye hakutaka uishi. usikurupuke kuishi eneo fulani kwa sababu zako wewe bila kibali kutoka kwa Mungu. Waombee wanao pia wasikimbilie kuishi maeneo ambayo Mungu hakutaka waishi. Naamini umeuelewa ujumbe huu tokea ulipoanza kuusoma. Mungu akubariki sana.

Kitabu hiki kimepigwa chapa na: Yamala Multimedia | P.O Box 306 Mbeya | 0784801900 | info@yamala.co.tz | www.yamala.co.tz